



**MUONGOZO
WA
SHUGHULI ZA ZAKA
ZANZIBAR**

**Umeandaliwa na
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana
Zanzibar**

1432/2011

DIBAJI

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote. Sala na Salaam zimshukie Mtukufu wa daraja, Mtume wetu na kigezo chetu, Nabii Muhammad (S.A.W). pamoja na wafuasi wake wote hadi kitakaposimama kiama. Ama baada ya hayo.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua juhudini kubwa ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi wake. Mipango na mikakati mingi imefanyika ikiwemo Dira 2020 na Mpango wa Kukuza na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA). Utaratibu wa Zaka katika jamii ya Kiislamu ni msingi imara katika kufanikisha malengo ya mipango hii. Kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na jumuiya na taasisi mbali mbali za Kiislamu za Zanzibar, imeonekana kuwa upo umuhimu mkubwa wa kujumuisha utaratibu wa Zaka katika juhudini hizo hasa kwa kuzingatia mazingira ya Zanzibar.

Jumuiya na Viongozi wa kidini wana nafasi kubwa zaidi ya kuendeleza utaratibu huu kwa kuweka mfumo mzuri wa Zaka ili ukidhi makusudio ya Sheria ya Kiislamu. Kwa mantiki hii, muongozo huu umetayarishwa ili kuwasaidia viongozi wa dini, Waislamu na wote wanaotaka kufaidika na utaratibu wa Muumba ili kuwa na elimu sahihi kuhusu Zaka kwa kulingana na wakati uliopo. Kufanya hivyo kutawasaidia wawe mstari wa mbele katika kuelimisha, kushajiisha, kusimamia na kutekeleza shughuli za Zaka ili itoe mchango wake katika juhudini za kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Hivyo muongozo huu ni wetu sote. Maelekezo yetu ya kuwataka watu wafuate miongozo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuwa wakweli, waaminifu, waadilifu, wenye upendo na huruma, lazima yaunganishwe na mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini kupitia Zaka, sadaka na taratibu nyenginezo zilizowekwa na Uislamu.

Manufaa ya muongozo huu yatategemea kwa kiasi kikubwa jinsi waumini watakavyokuwa makini na kuufanya kazi. Jukumu kubwa kwa waumini, Jumuiya na Taasisi za Kiislamu ni kuhakikisha kuwa muongozo huu unafanyiwa kazi ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana itahakikisha kwamba inawajengea uwezo wa kutosha wahusika wote ili waweze kuutumia muongozo huu kwa ufanisi mkubwa. Jitihada na mashirikiano yanahitajika ili kujenga jamii ya Wazanzibari iliyobora kiimani na kimaadili na wakati huo huo kufanikisha Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini.

Sh. Abdulla Talib Abdulla
Katibu Mtendaji,
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana,
Zanzibar

SHUKRANI

Shukran zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwafikisha kuandaa Muongozo huu. Kwa kuitikia kauli ya Mtume (S.A.W): ((لَا يَشْكُرُ اللَّهُ مَنْ لَا يَشْكُرُ النَّاسَ)) "Hamshukuru Mwenyezi Mungu asiyewashukuru watu" (*Imepokewa na Ahmad, Abu Daud na Ibnu Hibani*); tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Taasisi na Jumuiya za Kiislamu za Zanzibar, masheikh, wataalamu na waumini wote walioshiriki kwa namna yo yote ile katika kufanikisha kukamilika kwa Muongozo huu. Nafasi haitoshi kuwataja wote lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu anawajua na ndiye atakayewalipa.

Tunaishukuru Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuratibu suala hili la utayarishaji wa muongozo huu. Uandishi wa muongozo huu usingeweze kana pasina juhud kubwa zilizofanywa na Kamati ya Ushauri iliyowashirikisha: Sheikh Abdulla Talib Abdulla, Dr.Hamed Rashid Hikmany, Sheikh Ali Aboud Mzee na Sheikh Nassor Ameir Tajo. Aidha tunamshukuru Maalim Mohammed Ali Mohammed (Maalim Ugoda) kwa kazi ya kuhariri muongozo huu, na Shirika la Africa Muslims Agency kwa kufadhili uchapaji wake.

Tunakushukuruni nyote na kuthamini juhud zenu zilizopelekeea kukamilika Muongozo huu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Atupe tawfiki ya kuufanya kazi.

Dr. Muhammad Hafidh Khalfan.

Mwenyekiti

Kamati ya Ushauri.

YALIYOMO

| | |
|-------------------------|---|
| Dibaji..... | 1 |
| Shukrani..... | 2 |
| Yaliyomo..... | 3 |
| Ufupisho wa Maneno..... | 6 |
| Maana ya Maneno..... | 6 |

UTANGULIZI NA USULI

| | |
|--------------------------------|---|
| Historia ya Zaka Zanzibar..... | 8 |
|--------------------------------|---|

SURA YA KWANZA

| | |
|--|----|
| Maelezo ya Zaka na Misingi yake..... | 12 |
| Maana ya Zaka..... | 12 |
| Hukumu ya Zaka..... | 12 |
| Adhabu ya Asiyetoa Zaka..... | 12 |
| Hekma ya Kufaradhishwa Zaka:..... | 13 |
| Sharti za Kuwajibika kwa Zaka..... | 14 |
| Sharti za Mtoaji..... | 14 |
| Sharti za Mali Inayotolewa Zaka..... | 15 |
| Mali Zinazopaswa Kutolewa Zaka..... | 16 |
| Zaka ya Dhahabu na Fedha..... | 16 |
| Dalili ya Kuwajibikiwa na Zaka..... | 16 |
| Sharti za Kuwajibika Zaka yake..... | 17 |
| Kiwango cha Kutolewa Zaka..... | 17 |
| Zaka ya Mapambo..... | 17 |
| Zaka ya Pesa (Shillingi, Dola, Yuro, Riyale nk)..... | 18 |
| Hukumu Zinazoambatana na Zaka ya Dhahabu na Fedha..... | 18 |
| Zaka ya Wanyama..... | 19 |
| Dalili ya Kuwajibikiwa na Zaka ya Wanyama..... | 19 |
| Zaka ya Ngamia..... | 19 |
| Zaka ya Ng'ombe..... | 20 |

| | |
|--|----|
| Zaka ya Mbuzi na Kondoo | 21 |
| Hukumu ya Wanyama Wasiochungwa..... | 21 |
| Hukumu ya Wanyama wa Kazi..... | 21 |
| Wanyama Wengineo..... | 22 |
| Hukumu Zinazoambatana na Zaka ya Wanyama..... | 22 |
| Zaka ya Mazao na Matunda | 22 |
| Aina ya Mazao na Matunda Yanayopaswa Kutolewa Zaka..... | 22 |
| Wakati wa Kutolewa Zaka ya Mazao na Matunda..... | 23 |
| Kiwango cha Zaka | 23 |
| Hukumu Zinazofungamana na Zaka ya Matunda na Mazao..... | 23 |
| Zaka ya Mali ya Biashara..... | 25 |
| Makusudio ya Mali hii na Dalili ya Kuwajibika Zaka..... | 25 |
| Namna ya Kuvitolea Zaka..... | 25 |
| Zaka ya Mapato na Kitega Uchumi..... | 25 |
| Hukumu Zinazohusiana na Zaka ya Biashara..... | 25 |
| Zaka ya Hisa na Hati za Hazina..... | 27 |
| Hisa na Hukumu yake | 27 |
| Namna ya Kutoa Zaka ya Hisa..... | 27 |
| Hati za Hazina..... | 28 |
| Hukumu ya Hati za Hazina na Namna ya Kuzitolea Zaka..... | 28 |
| Tofauti kati ya Hisa na Hati za Hazina..... | 28 |
| Zakatul-Fitri..... | 29 |
| Hukumu yake..... | 29 |
| Wakati wa Kuwajibika Kutolewa..... | 29 |
| Kiwango Kinachotolewa..... | 29 |
| Anayestahiki Kupewa Zakatul-Fitri..... | 30 |
| Mambo Muhimu ya Kuzingatia..... | 30 |

SURA YA PILI

| | |
|--|----|
| Kugawa na kuzalisha Mali ya Zaka | 32 |
| Ugawaji wa Mali za Zaka..... | 32 |

| | |
|---|----|
| Wanaostahiki Kupewa Zaka..... | 32 |
| Namna Zaka Inavyotolewa..... | 33 |
| Utoaji wa Zaka kwa Mali za Wakfu Maalumu..... | 35 |
| Kuwekeza Katika Mali za Zaka..... | 36 |
| Misingi ya Kisheria Katika Uwekezaji..... | 36 |
| Kusaidia kwa Mkopo Nafuu | 36 |
| Kodi ya Kufanyakazi..... | 36 |
| Kodi Inayomalizika kwa Kumilikisha..... | 37 |
| Kuingia Katika Ushirika..... | 37 |
| Ushirika wa Kudumu..... | 37 |
| Ushirika Unaomalizika kwa Kumilikisha..... | 37 |
| Kusaidia kwa Kufanya Biashara ya Pamoja (<i>Mudharaba</i>)..... | 38 |
| Mudharaba wa Kudumu..... | 38 |
| Mudharaba Unaomalizika kwa Kumilikisha..... | 38 |
| Kusaidiwa kwa Mkopo Mwema(Qardhun-Hassan) | 38 |
| Miradi Inayostahiki Kupewa Kipaumbele | 38 |

SURA YA TATU

| | |
|--|-----------|
| Diwani ya Zaka..... | 40 |
| Muundo na Malengo ya Diwani | 40 |
| Dira ya Diwani..... | 41 |
| Hatua za Ukusanyaji, Ugawaji na Uwekezaji..... | 42 |
| Njia Zitakazotumika Katika Kukusanya Zaka..... | 42 |
| Njia Zitakazotumika Katika Kugawa Zaka..... | 43 |
| Kumbukumbu na Nyaraka Muhimu..... | 43 |
| Hitimisho..... | 43 |
| Viambatisho | 45 |

UFUPISHO WA MANENO

R.A Radhiyallahu Anhu (au anha kwa mwanamke)

S.A.W Salallahu Aleyhi Wasalam

S.W Subhaanahu Wataala

MAANA YA MANENO

| | |
|--------------------------|--|
| Amil | Anaefanya kazi ya kukusanya na kugawa Zaka. |
| Baitul-maal | Hazina ya mali ya waislamu. |
| Binti labuni | Ngamia jike alietimiza miaka miwili na kuingia wa tatu. |
| Binti makhadhi | Ngamia jike alietimiza mwaka mmoja na kuingia wa pili |
| Bodi | Bodi ya Uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. |
| Diwani | Diwani ya Zaka. |
| Fat-wa | Muongozo wa Kisheria kuhusu hukumu ya jambo. |
| Fisabilillah | Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. |
| Gharim | Aliyetopewa na madeni. |
| Hadithi | Yaliyopokewa kutoka kwa Mtume katika kauli au kitendo au ikrari. |
| Hiba | Ni kumgaia (kumtunuku) mtu kitu kwa ajili ya kujenga mapenzi baina yao. |
| Hiqqa. | Ngamia jike alietimiza miaka mitatu na kuingia wa nne. |
| Ibnu Sabil | Msafiri alieharibikiwa akawa hana cha jumfikisha anakokwenda wala anakotoka. |
| Ijmaa | Makubaliano ya wanachuoni wote wa zama husika juu ya hukumu ya kisheria. |
| Jadhaa. | Ngamia jike alietimiza miaka minne na kuingia wa tano. |
| Katibu Mtendaji | Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. |
| Kadhi wa Ruf | Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Rufaa Pemba. |
| Lajna | Kamati. |
| Muallafa | Mtu aliyeingia katika Uislamu na ikawa imani yake haijawa thabiti |
| Mudiri diwani | Kiongozi wa diwani. |
| Niswabu | Kiwango maalum kilichowekwa na Sharia. |
| Radhiyallahu Anhu | Mwenyezi Mungu amridhie. |
| Riqaab | Kumtoa mtu utumwani. |
| Sadaka | Ni kumgaia (kumtunuku) mtu kitu kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. |
| Salallahu Aleyhi Wasalam | Sala na Salamu za Mwenyezi Mungu Mtukufu zimshukie. |

| | |
|--------------------|---|
| Sharia | Sheria ya Kiislamu. |
| Subhaanahu Wataala | Aliyetakasika na Aliyemtukufu. |
| Sunna | Yote yaliyothibiti kutoka kwa Mtume (S.A.W) kwa kauli, kitendo, ikrari au sifa. |
| Tabii | Ng'ombe alietimiza mwaka na kuingia wa pili. |
| Musinna | Ng'ombe alietimiza miaka miwili na kuingia watatu. |
| Wakfu | Ni kufunga umiliki wa kitu na kuachia manufaa yake kwa jambo la kheri kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. |
| Waziri | Waziri anaehusiana na sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. |

UTANGULIZI NA USULI

HISTORIA YA ZAKA ZANZIBAR

Zaka ni moja kati ya nguzo tano za Kiislamu. Kwa msingi huo, historia ya shughuli za Zaka nchini mwetu inakwenda sambamba na kuingia kwa Uislamu hapa Zanzibar. Waislamu wa Zanzibar wamekuwa wakitoa na kupokea Zaka na sadaka tokea zamani ingawa utafiti wa kina juu ya suala hili haujafanyika.

Inasemekana kuwa mara nyingi masheikh ndio waliokuwa wakisimamia shughuli hizi za Zaka kwa kupiga hesabu zake, kukusanya na kugawa kwa wahusika. Zipo simulizi kuwa Makadhi Wakuu pia walismamia shughuli za Zaka ingawa sheria maalumu iliyoongoza mambo ya Zaka hajjulikani kama ilikuwepo au la.

Ili kuleta ufanisi katika shughuli za Zaka, aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhajj Aboud Jumbe Mwinyi aliunda Kamati ya Zaka na Sadaka ya Zanzibar mwishoni mwa miaka ya sabiini. Kamati hii ilikuwa chini ya Kadhi Mkuu na katibu wake alikuwa ni marehemu Sheikh Mwarabu Khalfani, pia ilijumuisha maulamaa, wafanyabiashara na wasomi. Kamati ilifanya harakati nyingi za kheri; hata hivyo, utaratibu madhubuti wa Zaka haukuweza kusimamishwa.

Sheria namba 5 ya mwaka 1980 iliyoanzisha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iliweka moja kati ya majukumu ya Ofisi hii ni kusimamia shughuli za Zaka. Juhudi nyingi zilifanyika ili kuweka utaratibu mzuri wa kufanikisha mpango wa Zaka ikiwemo kuanzisha *baitul-maal* lakini mafanikio hayakuwa makubwa. Aidha ni watu wachache tu ndio waliokitumia chombo hicho kutoa Zaka huku wengi wao wakigawa wenyewe, wakiatumia watu, maustadh na wanachuoni waliowaamini au hawakutoa kabisa. Pia utaratibu wa ugawaji katika Kamisheni haukueleweka na haukizingatia makusudio ya Sharia bali iligaiwa kama sadaka nyenginezo ingawa yale makundi ya wanaostahiki kupewa Zaka yalizingatiwa kwa kiasi kikubwa.

Kwa mujibu wa sheria namba 2 ya 2007 iliyoanzisha upya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, suala la Zaka limepewa umuhimu zaidi. Sehemu ya Sita ya sheria hiyo vifungu namba 60 na 61 vimebainisha kuwa Kamisheni ina wajibu wa kusimamia shughuli za Zaka. Katika usimamizi huo Kamisheni imetakiwa kuhakikisha kuwa:-

- Jamii kwa ujumla ina elimu sahihi na ya kutosha kuhusiana na mambo yote ya Zaka.

- Mtu mwenye uwezo na anayetaka kutekeleza wajibu wa Zaka anasaidiwa ili atekeleze wajibu wake kama inavyoelekeza Sharia.
- Mali za Zaka zinasimamiwa vyema na kutumika kwa kuzingatia Sharia na taratibu za kidini zilizopo; na
- Taarifa za hesabu za Zaka zinatolewa kwa jamii mara kwa mara zikibainisha makusanyo na matumizi yake.

Kwa mujibu wa sheria hii taarifa zozote za Zaka zitakazowasilishwa Kamisheni kuhusiana na milki, mali, pesa au akaunti ya mtu ye yote zitahesabika kuwa ni siri kabisa. Hakuna Mamlaka yo yote isipokuwa Mahkama Kuu ya Zanzibar itakayokuwa na uwezo wa kuamuru kutolewa kwa taarifa hizo. Sheria hiyo imeweka wazi kuwa mtu ye yote atakayetoa taarifa hizo bila ya idhini ya Kamisheni atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani anaweza kutozwa faini isiyozidi shillingi milioni tano au kufungwa kwa muda usiozidi miaka miwili.

Kifungu cha 61 kinaipa uwezo Kamisheni kuunda chombo cha kusimamia shughuli hii ambacho kinaweza kuwashirikisha watu binafsi, makampuni, taasisi binafsi, jumuiya za kidini kwa namna ambavyo Kamisheni imeonelea iwe. Aidha Kamisheni imepewa uwezo wa kuiruhusu Jumuiya yo yote au Mfuko kukusanya au kugawa Zaka kwa Zanzibar nzima au katika eneo maalumu.

Ingawa Sheria hii ilianza kutumika mwaka 2007 lakini usimamizi wa Zaka haukupewa msisitizo na umuhimu unaostahiki. Utoaji wa Zaka kwa kiasi kikubwa unaonekana kuwa ni shughuli binafsi na ya hiari. Zipo taasisi na jumuiya nyingi za Kiislamu zinazokusanya na kugawa Zaka lakini mara nyingi shughuli hii hutajwa tu kuwa ni mionganini mwa malengo ya Jumuiya hizo. Aidha watoaji na wanufaika wa Zaka hizo aghalabu huwa ni wale wale watu walio karibu na jumuiya au taasisi hizo. Taarifa na kumbukumbu za utoaji na upokeaji huu pia huwa hazipatikani.

Wapo watu binafsi ambao pia wanafanya shughuli za kukusanya na kugawa Zaka katika utaratibu ambao mara nyingi unakuwa na dosari kadhaa. Kimsingi hali hii ni kinyume na lengo la Zaka. Vile vile wapo Waislamu wanaotoa mamilioni ya pesa katika sadaka lakini hakuna senti tano wanayoitoa katika Zaka.

Kama ambavyo wapo wanaotolea Zaka shilingi elfu kumi waliyodunduliza kwa mwaka mzima katika kipindi hiki ambacho fedha inayopaswa kutolewa (*niswabu*) inazidi 6,800,000/-.

Mwanzoni mwa mwaka 2011 zilianza kusajiliwa jumuiya makhsusi zisizo za kiserikali zenyе lengo la kutoa elimu ya Zaka na sadaka, kukusanya na kugawa Zaka na sadaka ndani ya Zanzibar na kushiriki katika kutoa huduma za kijamii na misaada ya kibinadamu ili kunyanya hali za wanajamii. Jumuiya kama hizi zinapaswa kuomba leseni ya kufanya shughuli hizo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ili ziweze kufanya shughuli zake kisheria.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenyе mfumo wa Umoja wa Kitaifa chini ya uongozi wa Alhajj Dr Ali Mohammed Shein imekuja na azma kubwa ya kuiweka ibada ya Zaka pahala pake inapostahiki. Utafiti wa awali uliofanyika ulibaini kuwa ingawa wapo baadhi ya watu wanaotoa Zaka katika nchi yetu, lakini idadi yao bado ni ndogo na utoaji wao umekuwa hauleti tija wala kukidhi mahitaji na malengo ya kisharia. Sababu kuu zilizopelekea hali hiyo ni :-

- i. Kukosekana kwa elimu ya kutosha kwa Watoaji, Wapokeaji, Taasisi na Jumuiya za Kiislamu na watu wanaokusanya na kugawa Zaka.
- ii. Kutokuwepo chombo madhubuti chenye kuaminika na chenye uwezo wa kuelimisha, kukusanya, kugawa na kuratibu shughuli za Zaka kwa mujibu wa mahitaji ya wakati tulionao.

Ili kutekeleza azma hii ya Serikali na kukabiliana na changamoto zilizopo, Wizara ya Katiba na Sheria kupitia Kamisheni ya Wakfu ilifanya yafuatayo:-

- i. Kufanya mazungumzo na watu binafsi, Taasisi na Jumuiya za Kiislamu hususan zinazokusanya na kugawa Zaka ili kupata maoni yao kuhusu namna bora ya usimamizi wa Zaka na uanzishwaji wa Diwani ya Zaka.
- ii. Kuandaa rasimu ya Muongozo wa kutolea Elimu ya Zaka ili uweze kutumiwa katika maeneo yote ya jamii yetu ikiwemo misikitini, madrasa, vyombo vy ya habari, ana kwa ana na mtu kujisomea mwenyewe.

- iii. Kukusanya maoni na ushauri wa waumini, wanachuoni, wasomi, Jumuiya na Taasisi za Kiislamu kuhusiana na Muongozo wa Elimu ya Zaka ili kuufanya uwe bora zaidi na unaoendana na mahitaji ya wakati tulionao.
- iv. Kuunda timu ya washauri iliyoshirikisha watu wanaoaminika na wenye taaluma na uzoefu wa kutosha katika Sharia, Fedha na Uchumi.
- v. Kuweka utaratibu wa kuundwa Diwani ya Zaka, kupendekeza muundo wake na kubuni njia za namna itakavyoshiriki katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umistikini.
- vi. Kuendelea kuhamasisha makundi mbali mbali ili wakubaliane na fikra ya kuundwa kwa Diwani ya Zaka na kushiriki kikamilifu katika ibada hii.

Suala la Zaka limekusanya mambo mengi yakiwemo ya kiroho, kiimani na taaluma ya kina ya Sharia za Kiislamu na mambo ya kiuchumi. Aidha uelimishaji wa Zaka inabidi ufanyike kwa upana zaidi ili kila mta aweze kufikishiwa ujumbe. Kwa mashirikiano ya dhati ya kila mmoja na waumini inawezekana kuunda utaratibu huu ambao utasaidia sana jamii katika kutuletea kheri za dunia na akhera.

SURA YA KWANZA

MAELEZO YA ZAKA NA MISINGI YAKE

Maana ya Zaka

Zaka ni neno lenye asili ya kiarabu na maana yake inakusanya ziada, baraka na usafi. Ama kisharia ni jina linalotumika kwa mali maalumu inayotolewa na mtu maalumu kwa kundi maalumu baada ya kufikia kiwango maalumu kwa kuambatana na nia na shuruti maalumu .

Hukumu ya Zaka

Zaka ni moja kati ya nguzo tano za Kiislamu, hivyo ni fardhi kutolewa na kila Muislamu, mwenye kumiliki mali iliyofikia kiwango umiliki uliotimia kisharia. Dalili ya ulazima wake ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu [وأقيموا الصلاة واعطوا الزكاة] (Na simamisheni Sala na toweni Zaka) [Suratul Baqara aya ya 43]. Katika sunna kuna hadithi nyingi ikiwemo hadithi iliyopokelewa na Imam Bukhari na Muslim isemayo: [وابياء الزكاة] - وذكر منها- [بني الإسلام على خمس] "Umejengwa Uislamu kwa mambo matano..." na ikatajwa kati ya hayo "na kutoa Zaka". Wanachuoni wote wanakubaliana juu ya ulazima huu, kiasi cha Khalifa Abubakar Siddik (R.A) kusema: (والله لو منعوني عقالا كانوا يؤدونه على عهد رسول الله لقتلتكم عليه) "Wallahi lau kama watanizuilia kamba ya ngamia (kigwe) ambayo walikuwa wakiitoa katika zama za Mtume (S.A.W) basi ningeliwapiga vita kwa hilo" (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Tirmidhiy na Nasai). Hakuna sahaba ye yote aliyempinga kwa kauli hiyo, hivyo ikahesabiwa kuwa ni Ijmaa.

Adhabu ya Asiyetoa Zaka

Muislamu ye yote anayemiliki mali ambayo inafikia kiwango cha kutolewa Zaka na akawa haitolei kwa makusudi wala hakuusia kutolewa mpaka akafa, basi Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuandalia adhabu inayoumiza kama alivyosema kwenye Kurani tukufu:

{والذين يكترون الذهب والفضة ولا ينفقونها في سبيل الله فبئر هم بعذاب أليم، يوم يحمى عليها في نار جهنم فتكوى بها جاههم وجنوبهم وظهورهم هذا ما كنزنتم لأنفسكم فذوقوا ما كنزنتم تكترون}

((Wale ambao wanakusanya dhahabu na fedha na wala hawazitowi katika njia ya Mwenyezi Mungu basi wape habari za adhabu inayoumiza (ambayo wameandaliwa). Siku (mali zao) zitakapotiwa katika moto wa Jahanamu na kwazo vikachomwa vipaji vyao vya nyuso na mbavu zao na migongo yao (huku wanasmibuliwa kwa kuambiwa) Haya ndio yale mliyojilimbikizia kwa ajili ya nafsi zenu basi onjeni (adhabu ya) yale mliyokuwa mkiyakusanya)) [Suratul Tawba aya ya 34 na 35].

Katika hadithi iliyosimuliwa na Abu Hureira (R.A), Mtume SAW amesema:

[من آتاه الله مالا فلم يهد زكعه مثل له يوم القيمة شجاع أفرع له زبيبتان يطوفه يوم القيمة ... ثم يقول أنا مالك أنا كنزةك] ثم
تل النبى - صلى الله عليه وسلم - { ولا يحسن الدين يدخلون بما عاتهم الله من فضله هو خيرا لهم بل هو شر لهم
سيطونون ما بخلوا به يوم القيمة... }

"Yule ambaye Mwenyezi Mungu atampa mali na akawa hakuitolea Zaka yake, basi itamjia siku ya kiama katika sura ya Shujaa Akraa (nyoka mkubwa na mwenye sumu kali) ana nukta mbili nyeusi juu ya macho yake (nayo nia alama ya nyoka wabaya) amzonge shingoni (amuadhibu) siku ya kiama ... kisha amwambie mimi ni mali yako mimi ni hazina yako". Kisha Mtume S.A.W akasoma ((Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao watafungwa kongwa (minyororo ya shingo) za yale waliyoyafanyia ubakhili siku ya kiama)). [Suratu Ala Imran aya ya 180] (Hadithi ameipokea Bukhari na Nasai).

Hii iliyotajwa ni adhabu ya akhera, lakini kwa upande wa dunia pia kuna adhabu nyingi zikiwemo kupungukiwa na baraka, neema na kheri katika hiyo mali na maisha kwa ujumla. Amesema Mtume S.A.W : [ولم يمنعوا زكاة أموالهم إلا منعوا القطر من السماء ولو لا البهائم لم يمطروا] "Na wala hawatozuia Zaka ya mali zao ila watazuiliwa mvua (ya kheri) na lau kama si wanyama basi wasingenyeshewa na mvua". (Imepokewa na Ibnu Majah na Hakim).

Hekma ya Kufaradhishwa Zaka

Kufaradhishwa kwa Zaka kuna hekma nyingi zikiwemo hizi zifuatazo:-

- a) Hakika kupenda mali ni sifa ya mwanadamu ambayo inaweza kumpelekea kuwa mtumwa wa matamanio ya kukusanya na kushikilia mali kwa kila hali. Hivyo imefaradhishwa Zaka ili kuisafisha nafsi na uchafu wa ubahili, tamaa na kupenda dunia. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {خذ من أموالهم صدقة تطهرهم وتزكيهم بها} (Chukua katika mali zao sadaka (Zaka illi) uwasafishe na uwatakase kwa ajili ya hiszo) [Suratul Tawba aya ya 103].
- b) Kutoa Zaka kunajenga mahusiano bora ya kijamii na mapenzi kwa sababu nafsi ya mwanadamu imejengwa kimaumbile kumpenda yule anayemfanyia wema. Hivyo kuitia Zaka Waislamu wataishi hali ya kuwa wanapendana na wameshikana kama jengo madhubuti ambalo kila sehemu inaipa nguvu nyenzake.

- c) Kutoa Zaka kunapelekea kuhakikisha maana ya ibada, kunyenyeka na kujisalimisha kulikotimia kwa Mola wa viumbe vyote. Tajiri anapotoa Zaka ya mali yake huwa anatekeleza amri ya dini, pia ni katika kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa neema aliyomruzuku. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: {لَئِنْ شَكَرْتُمْ لِأَزِيْدِنَّكُمْ} ((Mkinishukuru basi nitakuzidishieni)) [Suratul Ibrahim aya ya 7].
- d) Zaka inapelekea ustawi wa jamii na kupunguza tofauti baina ya makundi ya watu kwa kurahisisha mzunguko wa mali na kupelekea makundi ya wanyonge kupata rasilimali. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ} ((Ili (mali) isiwe ikizunguka baina ya matajiri tu mionganoni mwenu)). [Suratul Hashri aya ya 7].

Sharti za Kuwajibika kwa Zaka

Ili Zaka iwe ni sahihi ni lazima zipatikane sharti maalumu ambazo zinahusiana na mtoaji na nyengine zinahusiana na mali inayotolewa.

a. Sharti za Mtoaji

Wamewafikiana Wanachuoni kuwa hakika ya Zaka ni wajibu kwa Muislamu, aliye baleghe, mwenye akili timamu na mwenye kuimiliki mali umiliki uliokamilika. Asili ya mali ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kama alivyosema: {وَآتُوهُم مِنْ مَالِ اللَّهِ الَّذِي أَتَكُمْ} ((Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu aliyokupeni)) [Suratun Nur aya ya 33]. Hata hivyo, Yeye (S.W) ndie aliyeiumba na akawaruzuku waja wake kwa njia mbali mbali. Pamoja na sharti hizo kuna mambo yafuatayo ni muhimu kuyazingatia:-

- i. Kauli iliyo sahihi kuhusiana na mtoto mdogo au mgonjwa wa akili, ni kuwa Zaka inakuwa ni lazima katika mali zao na watatolewa na mawalii wao. Hii ni kwa sababu Zaka ni haki iliyofungamana na mali ya Muislamu na sio dhima (nafsi) yao.
- ii. Kwa upande wa madeni, kauli iliyo sahihi ni kuwa Zaka inamuwajibikia mkopeshaji kwa sababu yeche ndiye mmiliki halisi wa mali, hata kama hawezi kuitumia mali hiyo kwa vile imo mikononi mwa mkopeshwaji. Zaka ya deni itawajibika pale mkopeshwaji anapokuwa yumo katika ahadi ya kulipa. Ama mkopeshwaji anapofilisika na ikawa haitarajiji kulipa au akawa mgumu wa kulipa bila ya sababu zinazokubalika kisheria, hapo mkopeshaji anaweza kusimamisha kuitolea Zaka mali hiyo mpaka atakapolipwa.

- iii. Iwapo watashirikiana katika mali kiasi cha kuhesabika mali ile kuwa ni moja (kwa mfano mali ya ushirika), basi mali hiyo itawajibikiwa na Zaka ikifikia kiwango hata kama fungu la kila mmoja halijafikia kiwango cha Zaka. Hali hii ni sawa kama ushirika huo ni kwa urithi, biashara au umoja.
- iv. Mali za umma mfano mali za Serikali, mali zilizomo katika Baytul- Mali huwa hazitolewi Zaka kwa sababu hakuna anaezimiliki umiliki uliokamilika.
- v. Mali zilizowekwa wakfu kwa kundi kubwa maalumu mfano, masikini, mayatima, misikiti, madrasa huwa hazitolewi Zaka kwa vile wao wanamiliki manufaa tu na hawaimiliki mali ama anapoweke wa mtu mmoja makhsusi kwa mfano wakfu wa mtoto mmoja tu maalumu hapo utatolewa Zaka.
- vi. Pesa wanazohifadhiwa wafanyakazi katika mifuko maalumu mfano Mfuko wa Hifadhi ya Jamii zitaangaliwa hali ya mfuko. Iwapo pesa hizo zinahesabika kuwa ni haki halisi ya wanachama na wanaweza kuzitumia basi italazimika kutolewa Zaka ama ikihesabiwa muwa ni manufaa tu wanayopewa na Serikali au mashirika wanaweza kuzifuta wakati wowote basi itakuwa hawazimiliki na hapo haitolazimu kuzitolea Zaka.
- vii. Mali ya haramu kama vile ya wizi, unyang'anyi, rushwa na riba huwa hazitolewi Zaka kwa sababu aliezishikilia si zake kisheria na Uislamu unamtaka azirejeshe kwa mwenyewe.
- viii. Inasisitizwa kuwa mtoaji atie nia kuwa anatoa Zaka ilijo lazima kwake wakati wa kuitoa. Amesema Mtume (S.A.W): [إنما الأعمال بالنيات وإنما لكل امرءٍ ما نوى] “Bila shaka kila amali inafungamana na nia. Na hakika hila mtu (hulipwa) kwa lile alilonuia” (Wamewafikiana Bukhari na Muslim). Hivyo mtu akitoa bila ya kunuia kuwa anatekeleza fardhi ya Zaka haitotosheleza kuwa ametoa Zaka.

b. Sharti za Mali inayotolewa Zaka

Mali inayotolewa Zaka ni lazima itimize masharti yafuatayo:-

- i. **Namaa:** Mali iwe inaweza kuzidi kwa kuzaliana au kwa faida ya kibiashara au kiufundi au iwe inayoweza kuongezeka kihukumu kama vile dhahabu, fedha na fedha za makaratsi ambayo huweza kuongezeka kwa njia ya biashara. Sharti hili linazitoa mali zinazotumika kwa kujinufaisha tu na sio kwa uzalishaji mfano nyumba ya kuishi, kipando, chakula na zana za kufanyia kazi.

- ii. **Niswaab:** Kufikia kiwango maalumu ambacho kimewekwa na Sharia ya Kiislamu kwa kila fungu la mali katika mali zinazotolewa Zaka kama ilivyobainishwa na Mtume (S.A.W).
- iii. **Hawlaanil hawl.** Iwapo mali imefikia kiwango na ikapitiwa na mwaka wa Kiislamu (Hijiria) basi huwajibikiwa kutolewa Zaka. Hii ni kwa hadithi ya Mtume (S.A.W) aliposema: [لا زكاة في مال حتى يحول عليه الحول] “Hamna Zaka katika mali mpaka ipitiwe na mwaka”. (Imepokewa na Maliki na Darakutniy). Katika sharti hili hayaingii matunda na nafaka kwani hivyo hutolewa Zaka wakati wa mavuno kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { آتُوا حَقَهُ يَوْمَ حِصَادِهِ } (Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake)) [Suratul An-am aya ya 141].

Mali Zinazopaswa Kutolewa Zaka

Tunapoangalia katika Kurani tukufu tutakuta kuwa Zaka imezungumzwa bila ya kuelezwu masharti yake kwa urefu. Mengi ya hayo yanapatikana kwa kina katika Sunna za Mtume Muhammad (S.A.W). Kadhalika yapo machache yaliyothibiti katika makubaliano na ijithadi za wanachuoni. Mali zinazotolewa Zaka kwa ujumla ni dhahabu, fedha, mazao, matunda, mali ya biashara, madini na mali zinazopatikana katika ardhi. Mali nyenginezo zimetajwa kwa ujumla wake pale aliposema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { خذ من أموالهم صدقة تطهر هم وتركهم بها } ((Chukua katika mali zao sadaka (Zaka) ili uwasafishe na uwatakase kwayo)) [Suratul Tawba aya ya 103].

Zifuatazo ni aina za mali zinazopaswa kutolewa Zaka kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu:-

1. Zaka ya Dhahabu na Fedha

Aina ya kwanza ya mali inayopaswa kutolewa Zaka ni madini ya dhahabu na fedha

Dalili ya Kuwajibikiwa na Zaka

Dhahabu na fedha ndio msingi wa harakati za kibashara baina ya watu. Kwa maana hiyo vitu hivi ndio asili ya pesa na mali, na ndio sababu ikawajibishwa kutolewa Zaka. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {((Na wale wanaokusanya dhahabu na لا ينفقونها في سبيل الله فبئرهم بعذاب أليم fedha na wala wakawa hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu basi wabashirie adhabu inayoumiza))} [Suratul Tawba aya ya 36]. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifanya sababu ya kupata adhabu kwa mtu ni kutokutowa Zaka ya dhahabu na fedha alizozikusanya. Aidha amesema Mtume (S.A.W):

[ما من صاحب ذهب ولا فضة لا يؤدي منها حقها إلا إذا كان يوم القيمة صفت له صفائح من نار فلحمي عليها في نار جهنم فيكوى بها جنبه وجبينه وظهره].

"Hakuna mwenye kumiliki dhahabu wala fedha na akawa hatoi haki yake ila itakapofika siku ya kiama atavikwa shaba ya moto akokotwe kwayo katika moto wa Jahannamu na achomwe kwayo ubavu wake na paji lake la uso na mgongo wake". (Imepokewa na Muslim na Bayhakiy) Kadhalika Wanachuoni wamekubaliana kuhusu ulazima wa kutoa Zaka hii na kuhesabiwa kuwa ni ijmaa.

Sharti za Kuwajibika Zaka yake

Ili mtu alazimike kuitolea Zaka dhahabu na fedha ni lazima zipatikane sharti tatu zifuatazo:-

- i. Kufikia kiwango (Niswaab).
- ii. Kupitiwa na mwaka (Hawalaanil hawl).
- iii. Kuwa na umiliki uliokamilika (Milki taam).

Kiwango cha Kutolewa Zaka

Mtume (S.A.W) ametaja kiwango cha Zaka ya dhahabu na fedha pale aliposema:

[ليس فيما دون خمس أواق صدقة وليس فيما دون عشرين مقلاً صدقة "Hapana chini ya wakia tano sadaka na hapana chini ya mith-qala ishirini sadaka". (Imepokewa na Ahmad, Bukhari na Muslim). Hivyo kiwango cha Zaka ni takriban gramu 85 za dhahabu au gramu 595 za fedha. Dhahabu na fedha zinapofikia kiwango cha Zaka huwajibika kutolewa robo ya fungu la kumi ambazo ni sawa na asilimia mbili na nusu (2.5%).

Zaka ya Mapambo

Wamekubaliana wanachuoni kuwa mapambo ya dhahabu na fedha ambayo ni haramu kuyatumia basi yanalazimika kutolewa Zaka. Baadhi ya wanachuoni wanawajibisha Zaka katika mapambo ya dhahabu na fedha. Miongoni mwa dalili walizozitoa katika kuthibitisha hayo ni hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Bibi Aysha (R.A) amesema:

(دخلت على رسول الله - صلى الله عليه وسلم - وفي يدي فتحات من ورق، أو قالت من ذهب، فقال: ما هذا؟ قالت: أتزيز
لَكَ بِهِنْ، قَالَ: أتؤذِنَ زَكَاتَهُنَّ؟ قَالَتْ: لَا. قَالَ: حَسْبُكَ مِنَ النَّارِ)

" Nimeingia kwa Mtume (S.A.W) na mkononi mwangu mna bangili (au pete kubwa) za fedha – Au alisema dhahabu-. Akasema: Nini hii? Nikajibu ninazitumia kwa kujipamba kwa ajili yako. Akasema "Jee unavitolea Zaka yake". Nikajibu: Hapana. Akasema "Basi vinakutosha (kukuingiza) katika moto". (Imepokewa na Abu Daud, Darakutniy, Hakim na Bayhakiy).

Hata hivyo mwanamke yuko katika hiyari; akitaka atatoa Zaka katika sehemu ya mapambo yake baada ya kuyapima au atatoa kima chake kwa asilimia 2.5.

Mapambo yatalazimika kutolewa Zaka yakiwa na moja ya hali zifuatazo:-

- i. Yawe yamekusudiwa kuhifadhi mali (imekusudiwa kuweka akiba).
- ii. Yawe yamefanywa vyombo kama vile sahani, vikombe na upanga.
- iii. Matumizi yasiyofaa mfano mwanamme kujivekea mapambo ya kike kama vile cheni na lakti.
- iv. Anayojipamba kwayo mwanamke katika mapambo ya wanaume kama upanga na jambia.

Zaka ya Pesa (mfano wa Shilingi, Dola na Riyale)

Sarafu na karatasi zenyе thamani ya mali zinapofikia kiwango na kupitiwa na mwaka basi huwajibika kutolewa Zaka. Hii ni kwa sababu vitu hivyo vinasimama sehemu ya dhahabu na fedha kwa vile ni njia ya kubadilishana manufaa, na hutimia kwazo kuuza na kununua. Aidha hufanywa ni sababu ya kutimiza haki, kufidia dhalma na manufaa mengineyo. Hivyo inasihi kupanga Zaka ya pesa kwa kipimo cha dhahabu au kwa fedha. Wahakiki wengi wanapendekeza itumike dhahabu kwa kujua kiwango halisi cha pesa (niswaab) kwa sababu katika zama hizi ndiyo inayotumika kupima thamani ya vitu.

Hivyo mtu anapotaka kujua kama mali yake imefikia au haijafikia kiwango cha Zaka itambidi aulize thamani ya gramu 85 za dhahabu kwa mujibu wa thamani ya soko ilivyo kwa wakati huo. Kiwango anachotoa ni kwa hesabu ifuatayo:-

(Thamani ya MALI x 2.5% = ZAKA). Mfano anamiliki shillingi 10,000,000 atazidisha mara 2.5 na atapata jawabu la 25,000,000 kisha atagawa kwa 100. Jawabu atakalolipata litakuwa ndio kiwango kinachomlazimu kutoa. Kwa hapa kiwango hicho kitakuwa ni shillingi 250,000.

Hukumu Zinazoambatana na Zaka ya Dhahabu na Fedha

Zifuatazo ni hukumu zinazoambatana na Zaka ya Dhahabu na Fedha:-

- i. Madini yo yote yasiyokuwa dhahabu na fedha kama vile lulu, marijani, almasi na yakuti huwa hayatolewi Zaka ila yanapouzwa na hapo huingia katika Zaka ya mali ya biashara.
- ii. Mtu anapokuwa na dhahabu, fedha na pesa huweza kuchanganywa zote kwa pamoja katika kuangalia niswabu (kiwango) kwa sababu vyote ni jinsi moja ya vitu vya thamani.

- iii. Ikiwa mtu anatoa kima (yaani pesa) katika Zaka ya dhahabu au fedha aliyonayo, utoaji huo hautapunguza thamani ya dhahabu na fedha zilizobakia. Kwa hivyo itamlazimu kila mwaka aitowe kwa mujibu wa kima chake halisi.
- iv. Mali inayotolewa Zaka baada ya kufikia kiwango huchanganywa na mali nyengineyo na sio kila mali kufikia mwaka wake.

2. Zaka ya Wanyama

Wanyama wanaokusudiwa katika hesabu ya Zaka ni ngamia, ng'ombe, kondoo na mbuzi. Wanyama wote hawa wanapaswa kutolewa Zaka kwa makubaliano ya wanachuoni wote. Masharti ya ujumla kwa Zaka ya wanyama na haya yafuatayo:-

- i. Wafikie Kiwango.
- ii. Wapitiwe na mwaka.
- iii. Wawe ni wanaochungwa.

Dalili ya Kuwajibikiwa na Zaka ya Wanyama

Kuhusiana na Zaka ya ngamia imethibiti kuwa amesema Mtume (S.A.W): [ليس فيما دون خمس ذود صدقة] "Hakuna chini ya ngamia watano sadaka." (Wamewafikiana Bukhari na Muslim). Ama dalili ya Zaka ya n'gombe imechukuliwa kutokana na hadithi ya Abu Dhari (R.A) kuwa Mtume (S.A.W) amesema:

[والذى نفسي بيده ما من رجل تكون له إبل أو بقر أو غنم لا يؤدى حقها إلا أتى بها يوم القيمة أعظم ما تكون وأسمنه تطوه بأخلفها وتنطحه بقرونها كلما جازت آخرها وردت عليها أولها حتى يقضى بين الناس]

"Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake hakuna mtu ye yote ambaye atakuwa na ngamia au ng'ombe au kondoo na akawa hatoi haki yake isipokuwa watatolewa siku ya kiama wakiwa wakubwa na wanene kabisa na wawe wanamtimba kwa miguu yao na wanamchoma kwa pembe zao, kila anapomalizika wa mwisho wao huanza tena wa mwanzo wao mpaka watu watakapohukumiwa." (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Tirmidhiy, Nasai na Ibnu Majah). Vile vile imesimuliwa kuwa Mtume (S.A.W) amesema: [ليس فيما دون أربعين شاة صدقة]"Hakuna chini ya kondoo arubaini sadaka."

Zaka ya Ngamia

Ngamia wataanza kutolewa Zaka wakifikia watano. Utoaji wake utatofautiana kwa kutegemea idadi ya ngamia wenyewe kama ifuatavyo:-

- a. Zaka ya ngamia waliokuwa chini ya idadi ya mia na ishirini ni kama ifuatavyo:-
- kutoka 5 hadi 9 patatolewa mbuzi mmoja (asiepungua umri wa mwaka mmoja).
 - kutoka 10 hadi 14 patatolewa mbuzi wawili.
 - kutoka 15 hadi 19 patatolewa mbuzi watatu.
 - kutoka 20 hadi 24 patatolewa mbuzi wanne.
 - kutoka 25 hadi 35 patatolewa *binti makhadhi*.
 - kutoka 36 hadi 45 patatolewa *binti labuni* .
 - kutoka 46 hadi 60 patatolewa *hiqqa*.
 - kutoka 61 hadi 75 patatolewa *jadhaa*.
 - kutoka 76 hadi 90 patatolewa *binti labuni* wawili.
 - kutoka 91 hadi 120 patatolewa *hiqqa* wawili.
- b. Ngamia waliozidi mia na ishirini kwa kila hamsini patatolewa *hiqqa* mmoja, na kwa kila ngamia arubaini patatolewa *binti labuni* mmoja kama ifuatavyo:-
- kutoka 121 hadi 129 patatolewa *binti labuni* watatu.
 - kutoka 130 hadi 139 patatolewa *hiqqa* mmoja na *binti labuni* wawili.
 - kutoka 140 hadi 149 patatolewa *hiqqa* wawili na *binti labuni* mmoja.
 - kutoka 150 hadi 159 patatolewa *hiqqa* watatu.
 - kutoka 160 hadi 169 patatolewa *binti labuni* wanne.
 - kutoka 170 hadi 179 patatolewa *binti labuni* watatu na *hiqqa* mmoja.
 - kutoka 180 hadi 189 patatolewa *binti labuni* wanne pamoja na *hiqqa* wawili.
 - kutoka 190 hadi 199 patatolewa *hiqqa* watatu pamoja na *binti labuni* mmoja.
 - kutoka 200 hadi 209 patatolewa *hiqqa* wanne au *binti labuni* watano.

Zaka ya Ng'ombe

Ng'ombe wataanza kutolewa Zaka wakifika idadi ya thelathini na utoaji wake uko kama ifuatavyo:-

- a. Ng'ombe ambao idadi yake haikufikia 120 watatolewa Zaka kama ifuatavyo:-
- kutoka 30 hadi 39 patatolewa *tabii* mmoja.
 - kutoka 40 hadi 59 patatolewa *musinna* mmoja.
 - kutoka 60 hadi 69 patatolewa *tabii* wawili.

- kutoka 70 hadi 79 patatolewa *musinna* mmoja pamoja na *tabii* mmoja.
 - kutoka 80 hadi 89 patatolewa *musinna* wawili.
 - kutoka 90 hadi 99 patatolewa *tabii* watatu.
 - kutoka 100 hadi 119 patatolewa *musinna* mmoja pamoja na *tabii* wawili.
 - kutoka 120 na zaidi ya hapo patatolewa *musinna* watatu au *tabii* wanne.
- b. Ng'ombe waliopindukia 120 kwa kila 30 patatolewa Zaka ya *tabii* mmoja na kwa kila 40 patatolewa *musinna* mmoja.

Zaka ya Mbuzi na Kondoo

Kondoo na Mbuzi wataanza kutolewa Zaka wakifikia idadi ya arobaini. Kiwango cha Zaka inayotolewa kwa mbuzi na kondoo hakitafautiani na itakuwa kama ifuatavyo:-

- kutoka 40 hadi 120 patatolewa mbuzi mmoja.
- kutoka 121 hadi 200 patatolewa mbuzi wawili.
- kutoka 201 hadi 399 patatolewa mbuzi watatu.
- kutoka 400 hadi 499 patatolewa mbuzi wanne.
- kutoka 500 hadi 599 patatolewa mbuzi watano.
- kutoka 600 na zaidi ya hapo, kwa kila mbuzi 100 patatolewa mbuzi mmoja.

Hukumu ya Wanyama Wasiochungwa

Wanyama wasiochungwa ni wale ambao wanategemea kile wanacholetewa mabandani mwao na kupewa huduma maalumu na sio kupelekwa machungani tu. Wanyama hawa hawatolewi Zaka. Zaka huwajibika kwa wale wanaopelekwa machungani kujichumia na hawahitajii matunzo ya ziada. Ushahidi wa hayo ni barua ya Sayyidna Abubakar (R.A): [...] وَفِي صِدْقَةِ الْغُنْمِ فِي سَائِمَتْهَا ... "Katika Zaka ya kondoo wanawajibikiwa wanaokwenda machungani." (Imepokewa na Bukhari, Abu Daud, Nasai na ibnu Majah).

Hukumu ya Wanyama wa Kazi

Wanyama wanaotumika kufanya kazi kama vile kulima, kumwagilia maji na kubeba mizigo; Wanachuoni wametofautiana kama wanatolewa Zaka au la. Kauli iliyodhahiri ni kuwa hawatolewi Zaka kutokana na hadithi ya Mtume (S.A.W): [وَلَيْسَ عَلَى الْعِوَالِ شَيْءٌ] "Na hakuna katika (wanyama) wanaofanya kazi (Zaka) yo yote" (Imepokewa na Abu Daud).

Wanyama Wengineo

Wanyama wengineo wote wakiwemo sungura, punda na farasi huwa hawatolewi Zaka ila wanapowekwa kwa ajili ya biashara hapo hulazimika kutolewa Zaka ya biashara kwa kuangalia thamani yao na hutolewa asilimia 2.5.

Hukumu Zinazoambatana na Zaka ya Wanyama

Zaka ya wanyama inaambatana na hukumu zifuatazo:-

- a. Muislamu anayemiliki mifugo yote ya kondoo na mbuzi, anapotaka kuwatolea Zaka huwachanganya na kutoa kwa pamoja.
- b. Baadhi ya wanyama hawachukuliwi katika kukusanya Zaka. Wanyama hawa hujumuisha mtoto anayemuata mama yake na kunyonya, anayelea mtoto, aliyenona sana, dume la mbegu, mkongwe, alodhofu (utibo), mwenye ulemavu wenye aibu na anayependwa zaidi na mfugaji.

3. Zaka ya Mazao na Matunda

Ardhi ni moja kati ya neema kubwa za Mwenyezi Mungu. Ardhi huotesha miti na mimeya ambayo huotesha mazao kwa uwezo Wake (S.W). Mazao na Matunda hayo yakinikmia maasharti yanawayibikiwa kutolewa Zaka kutohana na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: { وَأَتُوا حِقَهَ يَوْمَ حَصَادِهِ } (Na toweni haki yake (katika) siku ya mavuno yake) Suratul Tawba aya ya 34. Aidha kauli yake Mtume (S.A.W) aliposema:

[فيما سقط السماء والعيون العشر، وما سقي بالدوالي والغرب نصف العشر] "Kwa yale yaliyomwagiliwa na mvua na chemchemu basi (yatolewe zaka ya) ush-ru (fungu la kumi au 10%) na yaliyomwagiliwa kwa ndoo na madumu basi (yatolewe) nusu ya ush-ru (nusu ya fungu la kumi au 5%)". (Imepokewa na Bukhari, Abu Daud, Tirmidhiy, Nasai na Ibnu Majah).

Aina ya Mazao na Matunda Yanayopaswa Kutolewa Zaka

Wanachuoni wamekubaliana kuwa ni lazima Zaka itolewe katika ngano, shairi, tende na zabibu vinapofikia kiwango. Kwa ujumla aina hizi za mazao huunganishwa na vyakula vyote vyaya nafaka vinavyoweza kuhifadhiwa muda mrefu katika vile vinavyooteshwa na ardhi. Hii ni kwa sababu moja ya hekma ya kufaradhishwa Zaka ni kuondosha dhiki katika jamii.

Hapana shaka kuwa haja ya mafukara kwa vyakula vilivyoitiwa maghalani ni kubwa zaidi kuliko wengineo. Hivyo chochote kile kinachoshibisha na kuweza kubaki kwa muda mrefu hulazimika kutolewa Zaka. Ama visivyoshibisha kama vile lozi, *njugu*, komamanga, au visivyoweza kuhifadhika kwa muda mrefu kama tikit na tundadamu huwa haviwajibiki kutolewa Zaka bali inapendeza kutolewa sadaka.

Wakati wa Kutolewa Zaka ya Mazao na Matunda

Zaka ya mazao na matunda inawajibika kutolewa wakati wa mavuno. Ushahidi wa hayo ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: { وَآتُوا حِقَهٍ يَوْمَ حِصَادِهِ } ((*Na toeni haki yake (katika) siku ya mavuno yake*)) (Suratul Tawba aya ya 34). Wala haishurutishwi kupitiwa na mwaka katika Zaka hii. Hivyo kama mazao yatavunwa mara mbili au zaidi katika mwaka mmoja basi itawajibika kutolewa Zaka yake kila mara madhali yamefikia kiwango.

Kiwango cha Zaka

Mtume (S.A.W) amesema kuhusiana na kiwango cha Zaka ya mazao: [ليس فيما دون خمسة أو سق صدقة] "Hakuna sadaka chini ya Ausuki tano" (Wamewafikiana Bukhari na Muslim). Wask moja ni sawa na pishi 60; na pishi moja ni sawa na vibaba vine. Hivyo, nafaka zitawajibika kutolewa Zaka zikifikia pishi 300 ambazo takriban ni kilogramu 650.

Chakula kinachotolewa baada ya kufikia kiwango kinatofautiana kwa kuzingatia utegemeaji wa maji ya mvua au umwagiliaji. Iwapo kimemwagiliwa kwa mvua, mito, madimbwi, chemchem na maziwa basi kiwango kinachotolewa ni asilimia 10. Ama iwapo kimemwagiliwa kwa kutumia wanyama au njia nyenginezo za kisasa zinazotumia gharama basi hutolewa asilimia 5.

Katika mazao ni miti ya porini ambayo huvunwa na kufanywa mbao na magogo. Wapo wanavyuoni wanaosema kuwa miti hii pia hutolewa Zaka wakati wa kukatwa kwake. Lakini iwapo miti itabadilika maumbile yake kwa kuwa kuni au makaa, basi hapo itatolewa Zaka sawa sawa na mali nyenginezo za biashara.

Hukumu Zinazofungamana na Zaka ya Matunda na Mazao

Zifuatazo ni hukumu zinazofungamana na Zaka ya Matunda na Mazao:-

- a. Iwapo mtu atakuwa na kilogramu 400 za mtama na kilogramu 250 za mahindi basi itamlazimikia kutoa Zaka. Hii ni kwa sababu vitakuwa ni sawa na kitu cha aina moja kutokana na kuwafikiana kwake katika manufaa. Ama tende na zabibu kila moja inajitegemea hivyo kila moja lazima ifikie kiwango cha peke yake.
- b. Mtu anapokuwa na shamba zaidi ya moja, atatoa Zaka baada ya kujumuisha mazao ya matunda na nafaka ya mashamba yote. Mfano shamba hili amepata mavuno yenze kilogramu 300 na shamba jengine 350 itahesabiwa yamefikiwa kiwango.
- c. Iwapo mtu hutegemea mvua na kumwagilia, basi Zaka yake hutoa kwa kuzingatia hali zote. Anatakiwa akadirie kwa uadilifu kile kilichopatikana kwa mvua kitolewe asilimia 10 na kilichopatikana kwa kumwagiliwa kitolewe asilimia 5.
- d. Iwapo mazao yataharibika kwa sababu za kimaumbile kama mvua, upopo baada ya kuwajibika Zaka itaangaliwa kama ifuatavyo:-
 - Iwapo yataharibika bila ya uzembe wa mmiliki basi yataangaliwa mazao yaliyobakia ikiwa hayafikii kiwango basi haitotolewa Zaka ama yakifikia kiwango cha kilo 650 basi yatatolewa Zaka hayo yaliyobakia tu na yaliyoharibika hayatatolewa Zaka.
 - Ama yakiharibika kwa uzembe au usiri wa mmiliki hapo itamlazimu kutoa kima chake kamili kwani bado Zaka itamlazimikia.
- e. Inajuzu kwa mwenye mali kula matunda na mazao ya shamba kabla ya mavuno rasmi, kama ambavyo inajuzu kuwapa watu wake, majirani, wageni n.k kwa kadiri ya haja bila ya kufanya israfu. Mazao haya hayatahesabiwa katika kiwango kinachowajibika Zaka.
- f. Inajuzu mmiliki kutoa thamani badala ya mazao ikiwa haja ya mafukara inahitajia zaidi pesa au kama kuna uzito kutoa mazao, ama iwapo haja ya mafukara ipo zaidi kwenye mazao basi ni lazima atoe mazao.
- g. Mkulima mwenye deni katika shamba lake litaangaliwa asili ya deni hilo; iwapo limetokana na kuimarisha mazao kwa mfano kununua mbolea, mbegu na kupalilia basi litatolewa deni kabla ya kutolewa Zaka. Ama ikiwa deni linatokana na mahitaji yake binafsi basi halitozingatiwa katika Zaka. `

4. Zaka ya Mali ya Biashara

Makusudio ya Mali hii na Dalili ya Kuwajibika Zaka

Mali ya biashara ni mali yoyote iliyowekwa kwa ajili ya biashara sawa kama ni vitu, wanyama au bidhaa ilimradi viwe vinahesabika kuwa ni mali kisharia. Dalili ya kuwajibika Zaka kwa mali hizi ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: { يَأْيُهَا الَّذِينَ آمَنُوا انفَقُوا مِنْ طَبِيعَاتِ مَا كَسَبُتُمْ ((Enyi mlionamini toeni katika vizuri mlivovichuma)) Suratul Baqara aya ya 367. Na hadithi iliyopokelewa na Samrat bin Jundub (R.A) kuwa: [كان رسول الله - صلى الله عليه وسلم - يأمرنا أن نخرج الصدقة مما نعد للبيع "Hakika ya Mtume S.A.W alikuwa anatuamrisha kuvitolea Zaka vile tunavyoviweka kwa ajili ya kuuza." (Imepokewa na Abu Daud, Twabaraniy na Darakutniy). Pia Wanachuoni wote wamekubaliana kuhusiana na Zaka hii hivyo ikawa ni Ijmaa.

Namna ya Kuvitolea Zaka

Mali inapofikia kiwango na kuitikiwa na mwaka, mfanyabiashara anatakiwa afanye tathmini ya mali yote aliyoiveka kwa ajili ya biashara. Tathmini hiyo hufanywa kwa mujibu wa bei ya soko ya siku ile anayotaka kutolea Zaka. Kiwango kinachotolewa ni robo ya fungu la kumi ambayo ni asilimia 2.5.

Zaka ya Mapato na Kitega Uchumi

Iwapo mtu mmoja au kikundi wanamiliki mradi wa uzalishaji basi kinachohesabiwa katika kupanga kima cha kutoa Zaka ni ile faida iliyopatikana katika mradi huo. Hivyo thamani ya mashine, majengo na malighafi za kuendeshea mradi huwa hazihesabiwi. Faida itakayopatikana ikifikia kiwango na ikapitiwa na mwaka hapo italazimika hutolewa asilimia 2.5. Hukumu hii inahusisha miradi inayozalisha bidhaa za watu wengine kwa mfano mradi wa vyarahani vinavyoshonesha nguo kwa vitambaa vinavyoletwa na watu.

Iwapo mradi unazalisha na kuuza bidhaa zake wenyewe,basi thamani ya bidhaa na faida zitahesabiwa katika kufanya tathmini kama ilivyo katika Zaka ya biashara tulioitaja hapo kabla. Mfano mradi wa vyarahani unaonunua vitambaa na kuuza nguo.

Hukumu Zinazohusiana na Zaka ya Biashara

Zifuatazo ni hukumu zinazohusiana na zaka ya Biashara:-

- a. Vyombo na zana zinazotumika kwa maslahi ya biashara kama vile mizani za kupimia bidhaa, rafu, mafriji na gari za kubebaa bidhaa zinazouzwa hivi havitolewi Zaka.

- b. Mtoaji Zaka ana hiari baina ya kutoa Zaka kutokana na mali anayoifanyia biashara au kutoa thamani ya kima chake kwa pesa. Inapendeza kutoa kile kitu ambacho kitakuwa na maslahi zaidi kwa wanaostahiki kupewa Zaka.
- c. Mwenye kuwa na nyumba ya kukodisha itampasa kutoa Zaka kutokana na pesa anazokusanya katika kodi na hatoangalia thamani ya nyumba yenewe. Ama anapokusudia kuuza nyumba yenewe basi hapo nyumba itakuwa ni mali ya biashara ambayo itatathminiwa kama mali nyenginezo.
- d. Gari inayotumika kwa kuchukua abiria na bidhaa, hutolewa Zaka yake katika pato linalokusanya likifiki kiwango (cha kununua gramu 85 za dhahabu) na likipitiwa na mwaka. Ama gari zinazouzwa zitaingia katika Zaka ya biashara.
- e. Mfanyabiashara mwenye madeni (ya kudai na kudaiwa) Zaka yake atatoa kwa utaratibu ufuatao:- Atakesabu kima cha bidhaa zinazouzwa, atajumlisha na (+) faida iliyopatikana na kuhifadhiwa, atajumlisha na(+) madeni anayodai, kisha atatoa(-) madeni anayodaiwa. Jawabu anayopata atazidisha mara (x) 2.5%.

Mfano bidhaa zilizomo dukani zina thamani ya 10,000,000/-, faida na fedha iliyopatikana ni 300,000/- , wateja wanadaiwa 150,000/- na biashara ina deni la 50,000/-. Hesabu yake itakuwa $(10,000,000 + 300,000 + 150,000) = 10,450,000 - 50,000 = 10,400,000 \times 2.5$ gawa kwa 100 = 260,000. Hivyo Zaka itakayotolewa ni shillingi 260,000/-.

Deni linalozingatiwa hapa ni lile ambalo linategemewa kulipwa. Kwa maana hiyo wapo anayedaiwa amefilisika au hataki kulipa basi hicho kima anachodaiwi hakijumlis katika Zaka.

- f. Mtu asiyetoea Zaka ya mali yake kwa miaka kadhaa itamlazimu kwanza atubie kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kisha ajitahidi kukadiria kiwango anachodaiwa na kutoa kwa kipindi chote ambacho hakukitolea. Ataanzia katika mwaka anaofikiria kuwa alimiliki mali iliyofikia kiwango kisha atatoa kwa miaka yote ambayo hakuitolea Zaka.

5. Zaka ya Hisa na Hati za Hazina

Biashara ya hisa (*share*) na hati za hazina (*bond and treasury bill*) imekuwa maarufu katika zama zetu kiasi cha kuwekewa masoko na sheria maalum. Kwa msingi huo tumeona upo umuhimu wa kubainisha zaka yake na hukumu yake kisharia.

Hisa na Hukumu yake

Hisa ni sehemu ya umiliki inayotolewa na kampuni, shirika au ushirika ambao unabainisha kiwango cha haki ya umiliki katika rasilimali husika.

Kugawa rasilimali ya shirika katika hisa zilizo sawa ni jambo linalokubalika kisharia iwapo shughuli inayofanywa na hilo shirika inakubalika kisharia. Ama kuuza na kununua hisa kunakubalika iwapo sharti zifuatazo zitapatikana:-

- a. Shirika liwe halifanyi shughuli zinazokwenda kinyume kisharia kama kufanya biashara ya riba, ulevi, kamari na udanganyifu.
- b. Kujulikana thamani ya rasilimali na faida inayopatikana .
- c. Kuweza kubainisha na kutofautisha baina ya pesa, dhahabu na fedha, zilizopo na bidhaa za kibashara.
- d. Iwe uuzaaji wa pesa, dhahabu na fedha unakwenda mkono kwa mkono, wenyewe kufanana na ulio sawa sawa kutokana na hadithi isemayo [الذهب بالذهب والفضة بالفضة ... يدا بيد مثلًا فمن زاد أو استزاد فقد أربى "Dhahabu kwa dhahabu, fedha kwa fedha... mkono kwa mkono, sawa kwa sawa anayezidisha au kutaka ziada basi amekwisha chukua riba".(Imepokewa na Ahmad, Muslim na Nasai)].

Namna ya Kutoa Zaka ya Hisa

Iwapo shirika lenye hisa linafanya biashara kwa kuuza na kununua, au linazalisha na kuuza basi Zaka inayotolewa katika hisa huhesabiwa kutoka katika mali ya shirika pamoja na faida yake. Hivyo itazingatiwa kima chake chote unapofika muda unaolazimika kutolewa Zaka. Iwapo itafikia kiwango na kupitiwa na mwaka basi inalazimika kutolewa Zaka ya robo ya fungu la kumi yaani asilimia mbili na nusu (2.5%).

Ama shirika ambalo halifanyi biashara bali hujishughulisha na kutoa huduma kama vile za usafiri, kupangisha nyumba na huduma za afya; basi inapotolewa Zaka yake huwa hazihesabiwi thamani ya hisa, bali kinachotolewa ni katika faida tu pamoja na kuzingatia sharti zilizotajwa hapo kabla. Iwapo shirika litakuwa linatoa Zaka kwa binafsi yake basi wenyewe hisa hawatalazimika kutoa kwa vile mali haitolewi Zaka mara mbili.

Hati za Hazina

Hati za hazina ni hati au cheki inayotolewa kwa mtu anayetoa fedha katika sehemu iliyotangaza kukopeshwa mfano benki, shirika na kampuni kwa sharti ya kutoa faida maalumu kila mwaka sawa kama mkopeshwaji huyo atapata faida au hasara.

Hukumu ya Hati za Hazina na Namna ya Kuzitolea Zaka

Hati za hazina zinachukua hukumu ya kumkopesha mtu. Hivyo, mali inayomstahikia mmiliki wa hati hizo ni ile alioikopesha tu na ndio atakayoitolea Zaka kwani ndio anayoimiliki kisheria. Mali hii ataiunganisha na mali zake nyengine anazozitolea Zaka. Ama ziada itakayotolewa kwa mujibu wa makubaliano yao hiyo ni riba iliyoharamishwa ambayo kisheria sio haki kuitoa wala kuipokea. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنَ الرِّبَا إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنُونَ. إِنْ لَمْ تَفْعِلُوا فَأَذْنُوا بِحَرْبٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَإِنْ تَبْتَمِ فَلَكُمْ رِءُوسُ أَمْوَالِكُمْ لَا تَظْلِمُونَ وَلَا تُظْلَمُونَ}

((Enyi mliaomini mcheni Mwenyezi Mungu na acheni yaliyobakia katika riba ikiwa mumeamini. Na kama hamtafanya (hivyo) basi fahamuni kuwa mtakuwa na vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mkiwa mumetubu basi mtapata rasilimali zenu, msidhulumu wala msidhulumiwe)) (Al-Baqarah 278-279).

Tofauti kati ya Hisa na Hati za Hazina

- a. Hisa ni sehemu ya rasilimali ya shirika ama hati ya hazina ni sehemu ya deni la shirika.
- b. Hisa inafungamana na shirika kwa kupata faida au hasara, ama hati ya hazina inapata faida maalumu inayojulikana na haiathiriki kwa shirika kuongezekewa na faida au kupata hasara.
- c. Hisa hairejeshwi kwa mwenyewe mpaka itakapopangwa hesabu. Ama hati ya hazina hurejeshwa ukifika muda uliowekwa.

6. Zakatul-Fitri

Zakatul-Fitri ni Zaka maalumu inayotolewa baada ya kumalizika mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Imeitwa hivyo kwa sababu inawajibika kwa kuingia siku ya Iddi-el-fitri. Pia inaitwa Zaka ya viwiliwili na

kufungua miili kwa sababu inawajibika kwa kila nafsi na sio katika mali. Zaka hii imefaradhishwa mwaka wa pili Hijiria baada ya kufaradhisha funga ya Ramadani.

Hukumu yake

Zakatul-Fitri ni wajibu kwa kila Muislamu mkubwa na mdogo, mwanamke na mwanamme, huru na mtumwa. Mtu inampasa ajitolee Zaka hii yeye mwenyewe na kila anayemlazimu kumuhudumia kwa mfano mke, watoto na watu wake wa nyumbani. Imepokewa kutoka kwa Abdullah ibnu Omar (R.A): [أن رسول الله – صلى الله عليه وسلم – فرض زكاة الفطر من رمضان، صاعاً من تمر، أو صاعاً من شعير، على كل حرّ أوعبد، ذكر أو أنثى من المسلمين]

“*Hakika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) amefaradhisha Zakatul-Fitri katika mwezi wa Ramadhani pishi ya tende au pishi ya shairi kwa kila aliye huru au mtumwa, mwanamme au mwanamke katika Waislamu.*” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Abu Daud, Tirmidhiy, Nasai na Ibu Majah).

Wakati wa Kuwajibika Kutolewa

Inawajibika Zakatul-Fitri kwa kila Muislamu kwa kutua jua siku ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani na muda wake unaendelea mpaka watu wanaporejea kutoka katika Sala ya Iddi. Watu wanapomaliza sala na kurejea majumbani, muda wake unakuwa umekwisha. Atakaiyetoa kabla ya sala basi itakuwa ametoa Zaka inayokubalika na atakayeitoa baada ya sala basi itahesabika kuwa ametoa sadaka tu kama zilivyo sadaka nyenginezo na sio Zakatul-Fitri.

Kiwango Kinachotolewa

Kuhusiana na kiwango kachotolewakika Zaka hii, imepokewa kutoka kwa ibnu Omar (R.A): [أن رسول الله – صلى الله عليه وسلم – فرض زكاة الفطر من رمضان، صاعاً من تمر، أو صاعاً من شعير، على كل حرّ أوعبد، ذكر أو أنثى من المسلمين]

“*Hakika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) amefaradhisha Zakatul-Fitri katika mwezi wa Ramadhani pishi ya tende au pishi ya shairi kwa kila aliye huru au mtumwa, mwanamme au mwanamke katika Waislamu.*” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Abu Daud, Tirmidhiy, Nasai na Ibu Majah). Hivyo hadithi imebainisha kuwa kinachohitajika kutolewa ni pishi ya chakula katika aina zilizotajwa. Aidha inajuzu kutolewa kwa vyakula vya nafaka kama vile mchele. Iwapo mtu atazidisha zaidi ya pishi basi atapata ujira wa alichokizidisha. Pishi ya mchele inakadiriwa kuwa ni kilogramu mbili na gramu baina ya 40-80 na hutolewa katika chakula kinacholiwa zaidi katika mji husika.

Anayestahiki Kupewa Zakatul-Fitri

Wanaopewa Zaka hii ni masikini na mafukara ili watoshelezwe na mahitaji ya chakula kwa siku ya Iddi. Aidha wanaotangulizwa katika kupewa ni watu wema, wacha Mungu na watu wa kheri. Wala hawapewi makundi sita yaliyobaki katika ya manane ya wanaostahiki kupewa Zaka ila mtu anapokuwa ni muhitaji katika siku ya Iddi. Pia inajuzu kumpa mtu mmoja zaidi ya pishi moja. Muislamu inampasa achukue juhudii ya kuwatafuta wanaostahiki kupewa Zaka hii.

Mambo Muhimu ya Kuzingatia

- a. Mtoto aliye tumboni hatolewi Zaka kwa sababu bado hajazaliwa. Ama mtoto atakayezaliwa muda mchache kabla ya kutua jua kwa siku ya mwisho ya Ramadhani yeye itawajibika atolewe Zaka. Iwapo atazaliwa baada ya kuzama jua hata kwa muda mchache katika siku hii ya mwisho ya Ramadhani hatawajibikiwa kutolewa Zaka.
- b. Mtu anapokufa muda mchache kabla ya kuzama jua katika siku ya mwisho ya Ramadhani hawajibikiwi kutolewa Zakatul-Fitri ama atakayekufa baada ya jua kuzama italazimika atolewe.
- c. Iwapo mtu yumo safarini inampasa atoe Zaka hii katika mji aliomo ila kukiwa na ugumu wa kutoa ugenini hapo ndio inampasa ausie kutolewa katika mji wake.
- d. Sunna zinaonesha kuwa katika Zakatul-Fitri kunatolewa chakula kwa sababu Mtume (S.A.W) ametaja vyakula katika hadithi zote zinazoelezea vitu vya kutolewa Zaka hii. Hata hivyo, wanachuoni wamejuzisha kutoa kima kwa thamani ya pesa ili yapatikane makusudio hasa ya Zaka hii ambayo ni kuwatoshaleza masikini na mahitaji yao katika siku hii kama alivyosema Mtume (S.A.W). Pamoja na hayo iwapo chakula kitakuwa kina shida kupatikana, mtu ambae anamiliki chakula itamlazimu atoe Zaka kwa chakula na sio kima chake kwa thamani ya pesa.
- e. Wameruhusu baadhi ya Wanachuoni kutanguliza utoaji wa Zakatul fitri kwa siku moja au mbili kwa kuchunga maslaha na hali za mafukara au hali ya mtoaji iwapo atashindwa kwa dharura zake kuitoa Zaka hii katika Siku ya Iddi. Aidha baadhi ya Wanachuoni wa Kishafii wameruhusu itolewe katika kipindi chote cha mwezi wa Ramadhani kwa kuchunga hali hizo hizo.

f. Kuna baadhi ya misikiti ambayo hukusanya Zaka hii na kuigawa kwa kuzingatia orodha ya wahitaji waliopo katika mji huo. Jambo hili ni jema na linasaidia katika kuratibu shughuli za Zaka hii ili watu wote wanaostahiki wapewe. Ni vyema Maimamu wakachukua juhudzi zaidi katika kulifanikisha hili lili lifanyike katika misikiti mingi zaidi. Kutokuratibiwa Zaka hii kunapelekea baadhi ya watu pengine walio wahitaji zaidi kukosa na wengine kupata kingi. Iwapo msikiti utaratibu ukusanyaji na ugawaji majina yatakusanywa mapema na kila Muislamu anaweza kutoa Zaka mapema na msikiti ukatoa kwa wote wanaostahiki katika wakati unaotakiwa.

SURA YA PILI

KUGAWA NA KUZALISHA MALI YA ZAKA

Ugawaji wa Mali za Zaka

Zaka ni ibada ambayo Muislamu anawajibika kuitoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu huku akijuwa kuwa ni fardhi kwake. Zaka ni haki wanayostahiki kupewa makundi manane maalumu ya watu waliotajwa katika Kurani tukufu. Kwa kuwa Uislamu ni dini ya zama na mazingira yote, atakaezingatia kwa kina atagundua kuwa makundi haya na mnyumbuliko wake unakusanya watu wote walio wahitaji na shughuli nydingi za kheri na ustawi wa jamii..

Mamlaka inayokusanya na kugawa Zaka kwa kiasi kikubwa inategemea watoaji Zaka. Kwa kadiri makusanyo yanavyokuwa makubwa ndivyo ugawanyi, ufadhilli na usaidizi wa watu, shughuli na miradi mingi unavyokuwa mkubwa. Hata hivyo, Mfuko wa Zaka unatakiwa uwe endelevu ili uweze kutekeleza kazi zake mwaka mzima na hususan pale panapokuwa na matukio ya dharura yakiwemo majanga. Kwa msingi huo, Mamlaka ya Zaka inatakiwa iwe na mipango ya kuzizalisha mali zake.

Ili shughuli za Zaka zifanyike kwa ufanisi, mchango wa taasisi mbali mbali za Kiserikali na Kiraia unahitajika. Mfumo wa Zaka hauondoshi dhamana na majukumu ya Serikali wala jumuiya nyenginezo zenye malengo ya kunufaisha umma. Kinachotakiwa ni mashirikiano ili kufikia lengo kwa pamoja. Serikali inapoweka sera bora za uchumi na kuvutia uwekezaji; inapotoa wananchi wenye elimu, ujuzi, afya njema, ari ya kujituma na uadilifu; na ikadumisha amani na mshikamano katika nchi hapana shaka mapato ya watu yatapanda na wengi watamiliki *niswab* na kuwajibika kutoa zaka.

Asasi za kiraia zikiwemo kampuni binafsi na Jumuiya nazo zina mchango mkubwa katika shughuli za Zaka. Asasi hizi husaidia kwa kutoa ajira, utaalamu, misaada na ushauri katika mambo mengi. Iwapo mtu anapata utaalamu au kazi inayompatia kipato cha kumtosheleza yeye na familia yake, anaweza akawa mtoa zaka. Aidha kupata misaada mbali mbali ya kiuchumi na kijamii kutoka katika vyanzo mbali mbali kunaipunguza mzigو Mamlaka ya Zaka na hivyo kuipa nafasi kushughulikia katika nyanja nyengine.

Wanaostahiki Kupewa Zaka

Mali inayokusanya kwa ajili ya Zaka wanapewa watu wa makundi maalumu aliyoyataja Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Kur-an tukufu kwa kusema

{ إنما الصدقات للقراء والمساكين والعاملين عليها والمؤلفة قلوبهم وفي الرقاب والغارمين وفي سبيل الله وابن السبيل فريضة من الله والله عالم حكيم }

((*Hakika sadaka (Zaka) hupewa mafakiri, na masikini na wanaozitumikia, na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu), na katika kuwapa uungwana watumwa, na katika kuwasaidia wenyе madeni na katika kusaidia mambo aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu na katika kupewa wasafiri walioharibikiwa. Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hekima*)) [Suratu-Tawba aya ya 60].

Kwa maana hiyo watu wanaostahiki kupewa Zaka ni makundi manane yafuatayo:-

- 1) Mafukara nao ni wale wasiopata hata nusu ya mahitaji yao ya lazima.
- 2) Masikini nao ni wale wasiokamilisha matumizi ya mahitaji yao ya lazima.
- 3) Wanaofanya kazi ya kukusanya na kugawa Zaka (*Amil*). Hii inaweza kuingiza pia gharama za uendeshaji katika taasisi zinazosimamia ukusanyaji ugawaji na uratibu wa Zaka.
- 4) Watu walioingia katika Uislamu na ikaonekana ipo haja ya kupewa msaada ili wapate moyo zaidi wa kuwemo katika Uislamu (*Muallafa*).
- 5) Watu ambao wanaingia katika istilahi ya kukombolewa kutoka utumwani (*Al-Riqaab*).
- 6) Watu wenyе madeni ambayo hawawezi kuyalipa na ikaonekana haja ya kusaidiwa kulipa (*Al-Gharim*).
- 7) Mambo ya kidini anayoyaridhia Mwenyezi Mungu Mtukufu na yanayopeleka mbele Uislamu na maendeleo ya Waislamu (*Fisabilillah*).
- 8) Msafiri aliyekatikiwa na njia kwa kuharibikiwa na mambo yake na akawa hana fedha za kumrejesha kwao (*Ibnu Sabil*).

Namna Zaka Inavyotolewa

Zaka itatolewa kwa utaratibu utakaowekwa na Mamlaka inayoshughulikia Zaka. Utaratibu huu unaweza kutofautiana kwa kuzingatia mazingira, pahala, hali na aina ya watu wanaopewa Zaka hiyo. Utaratibu ni lazima uzingatie lengo la zaka kwa kila kundi. Lengo la Zaka kwa masikini na mafukara ni kuwapa mtaji wa kuondosha umasikini na ufukara wao na sio kuwapa chakula au pesa za chai. Hivyo kiwango kinachotolewa kiendane na malengo ya Zaka. Aidha kunahitajika upatikane ushauri wa kuwaongoza wapewaji ili wazitumie vizuri fedha na mali wanazopewa katika kujiletea maendeleo na sio kuzifuja.

Utoaji unaweza kuwa katika hali mbali mbali kwa kuzingatia makundi zikiwemo hizi zifuatazo:-

✉ *Masikini na Mafukara*

- Misaada ya kujitosheleza kwa chakula.
- Misaada ya kujikwamua kiuchumi.
- Misaada ya kimatibabu.
- Kugharamia masomo.
- Misaada ya makaazi au kulipia kodi ya nyumba.
- Misaada ya dharura ikiwemo yanapotokea majanga ya kimaumbile.
- Misaada ya kimalezi au matunzo ya watoto.
- Misaada ya kuwezesha kuingia kwenye ndoa.
- Misaada ya kibiashara.
- Misaada ya ujuzi na uwezeshaji katika Ujasiriamali.

✉ *Muallafa*

- Msaada wa kielimu au mafunzo ya kitaaluma.
- Kuandaa au kuchapisha vitabu kwa ajili ya Waislamu wapya.
- Shughuli za ulinganiaji na tablighi kwa kundi hili.
- Misaada ya makaazi.
- Kuanzisha vituo vya kukaa na kutoa huduma za dharura.
- Misaada ya kuwajenga imani Waislamu.

✉ *Amil*

- Anakusudiwa mtu au Jumuiya inayokusanya au kugawa Zaka. Inachukuwa sehemu ya inachokusanya ili iweze kumudu gharama za uendeshaji.
- Aidha wanaingia wafanyakazi wa *Baitulmal na Taasisi inayoisimamia*.

✉ *Al- Riqab*

- Kusaidia mtu ambaye haelewi lolote kuhusiana na dini ili atoke ujingani.
- Gharama za kuwakomboa waislamu walio mikononi mwa maadui ima kimwili au kiakili.

- Kuwakomboa watu waliomo katika mazingira ya hatari mfano walioathirika na madawa ya kulevyo, waliomo katika biashara ya umalaya, tabia za ubaradhuli, na kadhalika.

 *Al-Gharimin*

- Misaada ya kulipia madeni yakimaisha sawa kama ni ya chakula, elimu, afya na nyumba.
- Gharama za mazishi.
- Misaada kwa wenye madeni ya kibashara mfano waliofilisika.

 *Fisabilillah*

- Kuratibu na kusimamia shughuli za daawa.
- Misaada ya kitaaluma.
- Kuendeleza na kuhifadhi Uislamu.

 *Ibnu Sabil*

- Kuwasaidia watu wasioweza kurejea kwao.
- Kuwasaidia wanaotaka kuanza safari za kheri.

Utoaji wa Zaka kwa Mali za Wakfu Maalumu

Wakfu ni kuifunga mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuacha manufaa yake yatumike kwa watu au shughuli maalum zinazokubalika kisheria. Mara nyingi wakfu wa kheri unaweza ukawekwa unufaishe makundi ya watu wanaostahiki kupewa Zaka. Ikitokea kuwepo wakfu wa masikini, mafakiri, walioharibikiwa au kundi lolote kati ya manane yanayostahiki kupokea Zaka, kinaweza kutumika kiwango maalum cha mali ya Zaka kwa kuusaidia wakfu huo ili utoe tija zaidi kwa makundi yanayostahiki kupewa Zaka. Kwani kutumia mali hiyo kwa kuimarisha mali ya wakfu wao ni sawa na kuwasaidia wanufaika wengi zaidi wa kundi hilo na kwa muda mrefu. Ni vyema ikaeleweka kuwa kuusaidia Wakfu kwa Zaka, sadaka au mchango wo wote hakutomfanya mtoaji huyo kuingia katika Wakfu huo au kutengua lolote katika wasia wa Wakfu husika.

Kuwekeza Katika Mali za Zaka

Ni vyema Mfuko wa Zaka ukawa na fedha ambazo zitawekezwa ili zижжалишэ na kuufanya Mfuko uwe endelevu katika kukidhi mahitaji ya wahusika na kuchagia maendeleo ya kijamii. Utaratibu huu umeweza kuwanufaisha watu wengi kama inavyofanya mifuko mingi inayokopesha kwa masharti nafuu. Katika utaratibu huu kinaweza kuazimwa kiwango maalumu katika Zaka inayokusanywa na kikatiwa katika mfuko wa maendeleo ya jamii. Hata hivyo, mfuko huu unatakiwa kuendeshwa kwa utaratibu wa Kisharia na kuyasaidia makundi manane husika.

Misingi ya Kisheria

Sharia ya Kiislamu imeweka kanuni nyingi za kiuchumi ambazo zinaweza kutumika ili kukidhi mahitaji ya maendeleo kwa wakati tulionao. Misingi mikuu ya uzalishaji katika Uislamu imejengwa kwa kanuni zisemazo:-

- a. Tija au faida itoke katika gharama na kujituma. Maana ya kanuni hii ni kuwa shughuli inayoleta tija ni lazima itokane na jasho la anaepata faida hiyo au uwezekano wa kula hasara ikiwa yeye atatoa mtaji wa shughuli hiyo.
- b. Unapopata maslahi ni lazima ujikubalishe kubeba na hasara zake.
- c. Ukopeshaji ulenge kusaidia na si kupata faida.

1- Kusaidia kwa Mkopo Nafuu

Inawezeka Mfuko wa Zaka kuwa na rasilimali kwa mfano fedha taslim, mashine, boti , gari na mradi ambavyo atakodishwa masikini kwa sharti la kuwa taswarufi (matumizi) ya mali hiyo yatakuwa mikononi mwa maskini na umiliki wa mali mikononi mwa Mfuko. Hali hii inaweza kuwa katika hali mbili :-

a. Kodi ya Kufanyakazi

Mfuko utaanzisha vitendea kazi na majengo mbali mbali kisha utawakodisha wale wateja kwa mujibu wa haja zao. Kwa maana hiyo unaweza kusaidia katika kazi zote za amali na biashara. Aidha unaweza kusaidia katika kuanzisha miradi ya nyumba za kupangisha, usafirishaji wa abiria na mizigo na hata miradi inayohusiana na vyumba au vyombo vya kutolea barafu.

Chini ya utaratibu huu, Mfuko utanunua au kutayarisha zana kwa mujibu wa sifa zinazotakiwa na mhitaji na unamkodisha huyo mhitaji kwa masharti na muda maalum utakaotajwa katika mkataba kwa kuzingatia aina

na thamani ya mali iliyotolewa. Katika muda wote ambao deni halijalipwa zana zinakuwa chini ya umiliki wa mfuko na haki ya matumizi ya zana zinakuwa kwa yule aliyekodishwa. Baada ya kumalizika muda wa kukodisha haki zote zinarejea katika Mfuko.

b. Kodi Inayomalizika kwa Kumilikisha

Katika hali hii aliyepewa mtaji atamilikishwa zana za kazi kwa kuongeza kiwango maalum cha mali ili kuzinunua zana baada ya kumalizika muda wa kodi. Kiwango hiki cha ziada anaweza kukitoa sambamba na kodi, baada ya kumalizika muda wa kodi au katika muda maalumu baada ya kumalizika mkataba wa kukodi.

2- Kuingia Katika Ushirika

Katika hali hii mfuko unatoa mtaji na kununua zana ambazo zinamiliikiwa kwa pamoja (ushirika) baina ya mfuko na mpewa mtaji. Mapato yanayopatikana katika ushirika huu hugaiwa baina ya Mfuko na fakiri au maskini aliyepewa mtaji kwa viwango maalumu walivyokubaliana wakati wa kufunga mkataba.

Mfano wa ushirika huu ni fundi masikini ambaye ana ujuzi na sehemu ya kuchongea lakini hamiliki mtaji wa kununulia vifaa vya kuchongea. Hivyo hufanya ushirika na Mfuko kwa Mfuko kutoa vifaa na zana na masikini kutoa sehemu ya kiwanda na ufundi wake. Ushirika huu unaweza kuwa wa hali mbili zifuatazo:-.

a. Ushirika wa Kudumu

Aina hii ya ushirika ni ile ambayo makubaliano na mgao utaendelea kuwepo madhali mradi unaendelea. Mradi ukisimama kwa namna yo yote faida na hasara zitagaiwa kwa mujibu wa makubaliano.

b. Ushirika Unaomalizika kwa Kumilikisha

Aina hii ni ile ambayo unapofikia muda maalumu wa ushirika, mkataba hubadilishwa na kupelekea umiliki kwa masikini aliyesaidiwa peke yake. Inayumkinika kwa Mfuko kuweka masharti maalumu wakati wa umilikishaji. Kwa mfano, kuanzisha mradi utakaowaajiri idadi maalumu ya masikini; baada ya muda Mfuko ukawaachia hisa zake katika huo mradi wale masikini. Aidha Mfuko unaweza kumuachia mshirika wake kwa sharti la kuwafunza idadi maalumu ya vijana kazi za ufundi kwa muda maalum.

3- Kusaidia kwa Kufanya Biashara ya Pamoja (*Mudharaba*)

Kwa vile wapo watu wengi ambao wana ujuzi au vipaji vya kufanya shughuli fulani, lakini hawana mitaji ya kuanzia shughuli hiyo. Mfuko wa Zaka unaweza kuondosha tatizo hilo. Hali hii inaweza kuwahuusu wafanyabiashara, wanafunzi waliomaliza vyuo vikuu katika fani za udaktari, ufamasia, uhandisi, ualimu au hata wenyewe vyeti vya vyuo vya amali wanapokuwa katika makundi ya wanaostahiki kupewa Zaka. Inawezekana akawa mtu mmoja au kikundi cha watu 3-10. Biashara hii ya “mudharaba” inaweza kuwa ya aina mbili:-

a) Mudharaba wa Kudumu

Aina hii ya mudharaba ni Mfuko kutoa mtaji na aliyesaidiwa kufanya kazi huku wakigawana mapato yanayopatikana kwa viwango maalumu walivyokubaliana kwa muda wote mradi utakapokuwa unaendelea.

b) Mudharaba Unaomalizika kwa Kumilikisha

Aina hii ya muudharaba inamalizika kwa yule aliyesaidiwa kumilikishwa mradi wote kwa masharti maalum. Mfano masikini waliosaidiwa kuanzisha zahanati au kununua kifaa cha kupimia maradhi fulani kutakiwa kutoa huduma bila ya malipo kwa mafakiri au aina maalumu ya watu kwa vigezo maalumu

4- Kusaidiwa kwa Mkopo Mwema(Qardhun-Hassan)

Wapo watu wanaofanya biashara ndogo ndogo au vikundi vinavyokopeshana bila ya riba. Vikundi na watu hawa mara nyingi huhitaji mikopo ili kuendeleza mitaji ya biashara na shughuli zao. Ingawa kurejeshwa mikopo hii mara nyengine huwa ni vigumu, lakini Mfuko unaweza kusaidia hasa pale itakapothibitika kuwa msaidiwa ni masikini au fakiri anayeitegemea njia hiyo tu (biashara hiyo) katika kukimu mahitaji yake ya kimaisha. Katika mikopo hii Mfuko utakuwa na hali mbili katika kushughulikia wale walioshindwa kulipa:-

- a) Kuwasamehe deni lote wale ambao wameshindwa kulipa kutokana na haja zilizowakabili.
- b) Kuwaongezea muda wa kulipa au kupunguza kima ikithibiti kuwa wana uwezo wa kulipa iwapo wataongezewa muda au watapunguziwa kima cha kulipa pindi wakiwekewa muda maalumu.

Miradi Inayostahiki Kupewa Kipaumbele

Kwa kuzingatia makusudio ya Sharia, ipo miradi inayohitaji kupewa kipaumbele zaidi kuliko mingine katika kuwekeza au kugawa mali za Zaka. Miradi hiyo ni kama ifuatayo:-

- **Miradi Yenye Manufaa Bora kwa Jamii:** Miradi hii ni ile yenye lengo la kupunguza makali ya maisha pale inapotokea misukosuko ya kiuchumi. Lengo kubwa la kusaidia miradi hii ni kuziba pengo lililosababishwa na misukosuko hiyo kwa wananchi ambaa hali zao za kimaisha ni duni. Vile vile inaingia miradi ya kitabibu, elimu, maji safi na salama na inayoshabihiana nayo.
- **Miradi Yenye Manufaa Kiuchumi:** Hii ni miradi yote itakayopelekea kupunguza umasikini na kuwafanya watu wawe na uwezo wa kutoa Zaka. Mfano wa miradi hii ni uwekezaji katika viwanda, uvuvi, kilimo, ufugaji, na biashara kuitia uwezeshaji wa wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati kwa kuwajengea uwezo kielimu na kifedha.
- **Miradi Inayoheshimu Misingi ya Kiislamu:** Mfuko wa Zaka hausaidii miradi yo yote inayoharibu kwa namna yo yote ile dini na misingi yake. Hivyo ni lazima mradi unaosaidiwa uwe halali kwa asilimia mia moja na usiwe na *shubha* yoyote.
- **Miradi ya Kazi za Amali:** Kwa vile ufundu ni jambo linalohitajika siku zote na lazima ujuzi uhifadhiwe na kuendelezwa hasa ule ambaa unasa haulika, miradi ya kazi za amali ni lazima ipewe kipaumbele. Miradi hiyo ni ile inayotumia rasilimali za ndani ikiwemo kundi kubwa la rasilimali watu lisilo na ajira wala ujuzi wa aina yo yote. Kadhalika miradi ya kutoa huduma hasa inapokuwa inahitajika katika soko la ajira na ghamama zake za uendeshaji ni ndogo mfano useremala, uashi, upishi, ushoni na inayofanana na hiyo.

SURA YA TATU

DIWANI YA ZAKA

Muundo na Malengo ya Diwani

Diwani ya Zaka ni kitengo kinachojitegemea chini ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ambacho kitashughulikia mambo yote yanayohusiana na Zaka. Katika utendaji wake Diwani itawashirikisha watu binafsi, jumuiya na asasi mbali mbali ili kujenga uadilifu, uwajibikaji, ukweli na uwazi wa hali ya juu. Itakuwa na wafanyakazi walioajiriwa na wa kujitolea. Diwani itakuwa na nguvu za kisheria na itafanya kazi ili kuhakikisha kuwa malengo yafuatayo yanafikiwa:-

- Kazi ya ukusanyaji na ugawaji wa Zaka na sadaka kwa wanaostahiki inafanya kwa mujibu wa Sharia.
- Jamii kwa ujumla ina elimu ya kutosha kuhusiana na mambo yote yanayohusiana na Zaka, Sadaka, Hiba na Kafara.
- Mtu mwenye uwezo na anayetaka kutekeleza wajibu wa Zaka anasaidiwa ili atekelze wajibu wake kama inavyoelekeza Sharia.
- Taasisi, Jumuiya na watu waadilifu tu ndio wanaopatiwa leseni za kukusanya na kugawa Zaka visiwani mwetu.
- Taasisi, Jumuiya na watu waliopewa leseni wanatekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria zilizopo na maadili mema ya Kiislamu.
- Mali za Zaka zinasimamiwa vyema na kutumika kwa kuzingatia Sharia na taratibu za kidini zilizopo.
- Mali za Zaka zinawekezwa kwa mujibu wa Sharia ili kuufanya Mfuko wa Zaka uwe endelevu.
- Ripoti na kumbukumbu za hesabu na shughuli za Zaka zinatolewa kwa jamii mara kwa mara zikibainisha makusanyo na matumizi yake.

Diwani itaongozwa na *Mudir* ambaye atateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Katibu Mtendaji. *Mudir* wa *Diwani* atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa diwani na atawajibika kwa Katibu Mtendaji. Mtu hatofaa kuwa *Mudir* wa *Diwani* isipokuwa awe ni Muislamu, mwenye tabia njema, uadilifu na elimu ya juu ya uchumi wa Kiislamu. Aidha awe hajafikishwa mahkamani kwa kosa lolote la ubadhirifu, wizi au hadaa,

Diwani itakuwa chini ya usimamizi wa *Lajna* maalumu itakayoundwa na Bodi ya Uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Lajna hii itakuwa na wajumbe wasiozidi wanane wakijumuisha mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha, Jumuiya za Kiislamu, Wanachuoni wa madhehebu za Kiislamu, Jumuiya za Kiraia na watoa Zaka wakubwa. Lajna itakuwa ndio Mshauri na Msimamizi Mkuu wa Diwani, na bila ya kuathiri kazi za ujumla itakuwa na kazi na uwezo ufuatao:-

- Kuidhinisha sera na mipango mikuu ya Diwani.
- Kuchunguza kila kitu kwa mujibu wa vipaumbele au vidhibiti vyta kisheria.
- Kutangaza kiwango cha kisheria cha Zaka.
- Kufanya kazi yo yote ili kufanikisha malengo ya Diwani.

Kutakuwa na *Kamati ya Fat-wa* ya Diwani itakayojumuisha wajumbe watano. Wawili kati yao watateuliwa na Mufti wa Zanzibar kutoka katika Baraza la Maulamaa lilioanzishwa kwa Sheria ya Mufti. Wajumbe wengine watateuliwa na Lajna kwa kushauriana na Katibu Mtendaji. Kamati ya Fatwa itahusika na kufanya utafiti juu ya mambo yote ya kisharia yanayohusiana na Diwani na kuyatolea maamuzi. Vile vile itakuwa na mawasiliano na mabaraza yanayosimamia shughuli za Zaka ili iweze kutambua fatwa, *ahkami* na mambo mapya yanayojiri katika fik-hi ya Zaka. Kamati ya Fat-wa pia itaratibu kazi ya ulinganiaji katika Zaka.

Kutakuwa na Kamati ya Utatuzi wa Migogoro inayohusiana na Zaka itakayoundwa na wajumbe watatu. Mwenyekiti wake atakuwa ni Kadhi Rufaa na wajumbe wawili mmoja akiwa ni Ulamaa wa Mahkama Kuu ya Zanzibar atakayeteuliwa na Waziri kwa kushauriana na Katibu Mtendaji na Mwanachuoni Mtaalamu wa Fik-hi ya Mali na muamalaati atakayeteuliwa na Bodi. Mizozo yote itakayohusiana na Zaka itasikilizwa na Kamati hii.

Kabla ya kuanza rasmi kwa Diwani ya Zaka shughuli zote zinazohusiana na Zaka zitaendelea kuratibiwa na Kitengo cha Shughuli za Dini kilichopo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Dira ya Diwani

Diwani ina dira ya kuwa taasisi bora kabisa ya Zaka na kituo muhimu cha kujenga na kuimarisha uchumi wa jamii kwa:-

- Kutoa huduma bora kabisa.

- Kuwa na usimamizi mzuri wa rasilimali.
- Matumizi ya teknolojia ya kisasa.
- Kuendeleza watendaji.
- Kujenga mahusiano mazuri kabisa pamoja washirika na makundi yote.

Hatua za Ukusanyaji, Ugawaji na Uwekezaji

Shughuli zote za kukusanya Zaka, kugawa na Kuwekeza kutapitia katika hatua zifuatazo:-

- **Mipango:** itakusanya maandalizi ya mipango ya kazi, makundi yanayokusudiwa kufikiwa, makisio ya matumizi, watendaji na vifaa vinavyohitajika, muda unaohitajika na matokeo yanayotarajiwa. Aidha itaandaa tafiti, mafunzo na sera za mahusiano ya nje na ndani.
- **Utekelezaji:** Kila sehemu kufanya majukumu yake iliyopangiwa na kushirikiana na taasisi nyengine kama vile benki, idara na taasisi za serikali, jumuiya na taasisi binafsi, vyombo vyahabari na watu binafsi.
- **Udhibiti na Tathmini:** Itakusanya ufuutiliaji na uandaaji wa taarifa na ripoti za kila siku, kila wiki, kila mwezi na kila mwaka.
- **Kuendeleza Mafanikio:** Kwa kutumia ufoefu, ujuzi na teknolojia mpya katika kuendeleza shughuli za Zaka.

Njia Zitakazotumika Katika Kukusanya Zaka

Ili kurahisisha makusanyo ya Zaka njia zifuatazo zitatumika:-

- Madirisha ya Washika fedha za Diwani na Kamisheni ya Wakfu.
- Kaunta za benki.
- Posta (Hundi, *Bank Draft, Money Order*).
- Kupitia mikato ya mshahara.
- Mawakala wa Diwani.
- Benki za Kiislamu.
- Kupitia Misikiti (Makhsusi kwa Zakatul- Fitri).
- Taarifa za simu, mitando na mapatano.

Njia Zitakazotumika Katika Kugawa Zaka

Kamisheni itagawa yenyewe Zaka na pia itatumia wawakilishi wengine wakiwemo:-

- Taasisi na mifuko ya Serikali.
- Jumuiya, taasisi na mifuko ya Kiislamu.
- Jumuiya na mawakala wa Zaka.
- Watu wenye kuaminika.

Kumbukumbu na Nyaraka Muhimu

Kutakuwa na fomu, nyaraka pamoja na kumbukumbu ambazo zitatumika katika shughuli mbali mbali za Zaka. Nyaraka na kumbukumbu hizi zinaweza kubadilishwa kwa kadiri mahitaji yatakapotokea. Kati ya nyaraka hizi ni kama ifuatavyo:-

- a. Masharti ya kusajiliwa na kufanya kazi ya ukusanyaji na ugawaji wa Zaka.
- b. Fomu ya kuomba kusajiliwa kusajiliwa kuwa mkusanyaji wa Zaka.
- c. Leseni ya kukusanya na kugawa Zaka.
- d. Orodha ya taasisi zinazokusanya Zaka pamoja na anuani zake, mawasiliano yake na nambari za akaunti zake.
- e. Takwimu za ukusanyaji wa Zaka kwa mwaka kwa kigao cha Zanzibar, Tanzania Bara na nje ya Tanzania.
- f. Takwimu za ukusanyaji wa Zaka kwa mwaka kwa Wilaya zote za Zanzibar.
- g. Takwimu za ukusanyaji wa Zaka kwa kuzingatia aina ya Zaka.
- h. Takwimu za ukusanyaji wa Zaka kwa kuzingatia orodha ya taasisi zinazokusanya Zaka.
- i. Takwimu za ugawaji wa Zaka kwa mwaka kwa Wilaya zote za Zanzibar.
- j. Takwimu za ugawaji wa Zaka kwa kuzingatia makundi ya wanaopokea Zaka.
- k. Takwimu za ugawaji wa Zaka kwa kupitia orodha ya taasisi za misaada ya kheri.

Hitimisho

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ikishirikiana na Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Zanzibar, imeandaa Muongozo huu wa Zaka ili kufanikisha mikakati yake ya kuimarisha hali za maisha ya wananchi wake kwa kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuwa na

utawala bora. Ili hilo lifanikiwe, mashirikiano kati ya Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na Jumuiya za Kiraia ni muhimu katika kusimamia utekelezaji wa nguzo hii muhimu ya Uislamu.

Makusanyo ya Zaka Zanzibar yanaweza kusaidia jitihada za Serikali katika kukuza uchumi na kupambana na umaskini pindi yakitumika vyema na kwa uadilifu. Hili likifanikiwa, pia litahamasisha watoaji Zaka. Hivyo, ni vyema makusanyo ya Zaka yakagaiwa kwa lengo la kuondosha/kupunguza umaskini kwa njia endelevu zitazokuwa na athari kwa wanaopewa bila kukiuka utaratibu ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu Ametuamrisha.

Imeshauriwa katika Muongozo huu kuwa ni vyema Mfuko wa Zaka ukawa na fedha ambazo zitawekezwa ili zижизлишне na kuufanya mfuko uwe endelevu katika kukidhi mahitaji ya wahusika kama Mwenyezi Mungu Mtukufu Alivyowataja na kuchangia maendeleo ya Waislamu. Utaratibu huu umeweza kuwanufaisha wengi kama inavyofanya mifuko mingi inayokopesha kwa masharti nafuu. Njia ni nyingi na hutegemea kiwango cha kiuchumi kilichofikiwa na nchi husika. Muongozo umetoa mifano mbalimbali ya kiuchumi na huduma za kijamii ambapo Maulamaa wa baadhi ya nchi za Kiislamu wametoa maoni yao kuhusu kujuzu kutumia makusanyo ya Zaka. Moja ya njia hizo ni kutoa mafunzo ya uzalishaji na nyenzo zake ili masikini na mafukara wasiokuwa na ajira waweze kujari wenyewe, na waweze kuongeza kipato chao cha kila siku na hatimaye nao wainuke na watoe Zaka.

Mwisho, sote popote tulipo tuna jukumu la kufanikisha utekelezaji wa Zaka kuanzia kuelimisha, kusimamia ukusanyaji na ugawaji wake kwa uadilifu katika nchi yetu. Hilo likifanyika, jitihada za Serikali kukuza uchumi na kupunguza umasikini zitafanikiwa haraka zaidi na kuwafanya Wazanzibari waishi maisha mazuri zaidi yatayofanikisha lengo la kuumbwa kwetu ambalo ni ibada kwa ufahamu wake mpana Kiislamu.

VIAMBATISHO



KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

DIWANI YA ZAKA

ZANZIBAR

MASHARTI YA KUSAJILIWA

NA KUFANYA KAZI YA UKUSANYAJI NA UGAWAJI ZAKA

Taasisi au Jumuiya inayotaka kuendesha shughuli za Zaka katika visiwa vya Zanzibar ni lazima ifungamane na sharti zifuatazo:-

1. Iwe ni taasisi ya Kiislamu iliyosajiliwa rasmi.
2. lombe ruhusa ya kukusanya Zaka ikibainisha eneo itakalofanyia kazi, aina ya Zaka itakayokusanya na kugawa.
3. Kuendesha shughuli za Zaka kwa mujibu wa taratibu za kiislamu na kufuata miongozo na kanuni nyenginezo zilizopo au zitakazobainishwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.
4. Kuwasilisha ripoti ya ukusanyaji na ugawaji wa Zaka kila unapofika mwisho wa mwezi wa Dhulhijja Hijiria (mwezi wa mwisho wa kalenda ya Kiislamu).
5. Kuhifadhi siri za watu au Taasisi zinazotoa Zaka kuhusiana na hali zao, mali zao, fedha, akauti, mapato, Zaka wanazotoa isipokuwa kwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.



KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

DIWANI YA ZAKA

ZANZIBAR

LESENI YA KUKUSANYA NA KUGAWA ZAKA

Hii ni kuthibitisha kuwa.....
yenye Makao yake.....na hati ya usajili namba.....
Imeruhusiwa kukusanya na kugawa Zaka,
kwa mujibu wa Sharia ya Kiislam na Kanuni zilizopo kuanzia leo tarehe
.....sawa na hadi.....sawa na.....
Katika eneo la

Wakati ikikabidhi hati hii yenye nambari Kamisheni inausia kumcha
Mwenyezi Mungu katika shughuli hii na kufuata kanuni zilizopo na mwenendo wa watu
wema waliopita.

Wallahu waliyyu tawiq

.....
Mudir
Diwani ya Zaka
Zanzibar

.....
Katibu Mtendaji
Kamisheni ya Wakfu/Amana
Zanzibar

Seal